# Nipashe

Jumatatu Aprili 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580204

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US







## 'Waume wa watu' kikwazo wajawazito kwenda kliniki


UKURASA 4

UKURASA 11


# Corona yatawala makanisani Pasaka

• **Maaskofu** wataka wananchi kuchukua hatua kujikinga, Mkuu wa KKKT ateta na JPM, mwingine aonya kuhusu hofu...


*Endelea ukurasa 2,3*




### BAA LA CORONA

**Watu walio katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya Covid -19 ni wazee, na walio kwenye uangalizi maalumu wa dawa (kama wenye magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, moyo, homa ya mapafu au saratani). Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) linaendelea kutafiti.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, akihubiri kwenye Ibada ya Jumapili ya Pasaka iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Dodoma Mjini jana. **PICHA: IBRAHIM HOSEPH**

## Mvua kunyesha siku nne mikoa 6


UKURASA 4





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store


## CAG afichua utata posho Naibu Waziri Ofisi ya Rais


UK.4


**MICHEZO** TSHABALALA AIONA SIMBA FAINALI CAF UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## JPM, Mkuu wa KKKT wateta kuhusu corona

**Na Godfrey Mushi,**

MOSHI

RAIS John Magufuli, jana alizungumza na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, kuhusiana na ugonjwa wa homa ya mapafu Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Askofu Dk. Shoo, ameeleza namna alivyofurahishwa na mazungumzo yake na Rais Magufuli, akimsisitiza kuhimiza waumini wa Kanisa hilo kuongeza umakini wa kuchukua tahadhari kuhusu maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu.

Akitoa salaam za Pasaka jana, katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini la Dayosisi ya Kaskazini, Askofu Dk. Shoo alisema katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli alimtaka kufikisha salamu zake za sikukuu ya Pasaka kwa waumini wote wa Kanisa hilo nchini.

"Nimeongea na Mheshimiwa Rais, anawatakia Pasaka njema, anawaomba na anasisitiza sana tuendelee kuchukua hatua za kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona," alisema Askofu Dk. Shoo na kuendelea."

"Mungu anajua mahangaiko yetu msiogope. Corona ipo tujihadhari, lakini pia Yesu Kristo yupo ambaye ni mshindi wa mauti."

Wakati anahubiri katika ibada ya Pasaka, Dk. Shoo aliwaeleza waumini wa KKKT kuwa kufufuka kwa Yesu Kristo ndio kiini cha imani waliyonayo Wakristo.

Alisema: Kwa sasa dunia inahuzunika, watu wamepoteza ndugu zao, wengi wanahofu, lakini ni lazima tuikabili hofu yetu.

"Kuna hofu kubwa ya kusambaa kwa virusi vya corona na kuongezeka vifo inatisha."



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina chonjo, akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara wa soko la Manzese (hawapo pichani), juu ya umuhimu wa kuweka maji katika ndoo za kunawia wateja kabla hawajaingia sokoni hapo ili kujikinga na virusi vya corona. **PICHA FRANK KAUNDULA**

# Corona yatawala makanisani Pasaka

**Na Waandishi wetu**

IBADA za Sikukuu ya Pasaka, jana zilitawaliwa na mahubiri ya kuwasihi wananchi kuchukua tahadhari, kumrudia Mungu na kuwalinda watoto dhidi ya corona.

Kadhalika, viongozi wa dini waliohubiri waliwataka wananchi kujitokeza kupata tiba na kujitenga wanapoona dalili huku wakipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua.

**IRINGA WATAKA UNYENYEKEVU**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, Blaston Gavile, ametaka Watanzania kujinyenyekeza na kumrudia Mungu kwa toba ili kuliepusha na corona.

Alisema unyenyekevu mbele ya Mungu unapaswa kufanyika ili Mungu aweze kuliepusha taifa na janga la corona .

"Tunaadhimisha sikukuu hii ya Pasaka wakati ambapo dunia nzima imejaa hofu na mahangaiko... tumeguswa na tutaguswa na janga hili, kwa namna moja ama nyingine tunahitaji kila tafakari na kufuata maelekezo ya serikali yetu na mamlaka za afya na sisi kama kanisa tumeshatuma kwa dayosisi zote maelekezo," alisema.

Aidha, tofauti na miaka mingine hakukuwa na wageni kutoka nje ya Usharika.

**KAHAMA WAMSIFU RAIS**

Mchungaji wa KKKT, Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Ushirika wa Agape, Daniel Mono, alisema Rais Magufuli anastahili sifa kutokana na ujasiri wake uliowafanya Watanzania kufanyakazi na kusali kwa tahadhari kubwa.

"Dunia imekuwa ndogo, kila mahali watu wanatafuta nafasi hawatoshi lakini Rais Magufuli amekuwa akiwatoa hofu na woga Watanzania kwa kutumia Theologia kubwa ambayo hata baadhi ya viongozi wameshindwa kuielewa na yapo baadhi ya makanisa yameshindwa kuendesha ibada kwa hofu," alisema Mchungaji Mono.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, akitoa salamu za Serikali, aliwataka wananchi kuendelea na kazi kwa tahadhari kubwa kwa kuwa hali za maisha ni lazima watoke kutafuta riziki tofauti na nchi zilizoendelea wanajiweza.

**ASKOFU AWAONYA WAFANYABIASHARA**

Askofu Mkuu wa makanisa ya Maombezi Tanzania, Living Mwambapa, amewataka wafanyabiashara wa maduka waliopo vijijini kutotanguliza maslahi mbele kwa kupandisha bei ya vifaa vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Badala yake amewataka kusaidia juhudi zinazofanywa na serikali ikiwa na kutoa elimu ya jinsi ya matumizi ya vifaa hivyo, juhudi hizo ziweze kuleta mafanikio ya ugonjwa huo kutoweka nchini

Alisema kuwa, wakati serikali ikifanya juhudi kubwa za kusambaza vifaa vya kujikinga ikiwamo na utoaji wa elimu, bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wa vijijini kwa upande wao wameona ni muda mzuri wa kupandisha juu bei ya vifaa hivyo, hali inayoonyesha wazi kukwamisha kutokomeza ugonjwa huo.

"Huko vijijini bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wanatumia mwanya wa ujio wa ugonjwa huu kutaka kukwamisha juhudi zinazofanywa na serikali za kuondoa ugonjwa huu, badala yake wao wanapandisha bei vifaa hivyo, hali inayoonyesha baadhi ya familia zitashindwa kutokana na gharama na hatimaye wakashindwa kutekeleza maagizo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka hayo ili kujua uhalisia.

**ARUSHA WAONYA WATOTO KUZURURA**

Paroko wa Kanisa la Utatu Mtakatifu Kwamurombo, jijini Arusha, Padri Peddy Castelino, aliwataka waumini kuwazuia watoto wao wasitoke nyumbani na kwenda kuzurura ovyo mtaani wakati huu wa tishio la corona.

Alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wazazi ambao ni waumini wake kuacha watoto wakizurura ovyo mitaani wakati huu ambao shule zimefungwa.

"Shule zimefungwa kwa sababu ya corona, hivyo siyo sababu ya kuwaacha watoto wazagae ovyo, hapana, na hata hapa kanisani muwaache nyumbani wapumzike wasije," alisema.

"Kama hakuna sababu ya kutoka nje msitoke, tulieni kwenye nyumba zenu msisubiri serikali ije kuwazuia ndani, chukueni hatua," alisema.

Katika Ibada hiyo, askari Polisi walionekana wakisimamia utaratibu wa waumini wanne kukaa benchi na waliozidi walitolewa nje ya kanisa na kusimamiwa katika umbali wa mita moja, huku wenye watoto wakitolewa nje ya kanisa kwa usalama wao.

**BABATI WATAKA HATUA ZA KISHERIA**

Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu, ameagiza kuchukuliwa hatua za kisheria watu wanaokaidi kunawa mikono kwenye maeneo ya kutolea huduma kwa kuwa wanakiuka maelekezo ya serikali kupambana na corona.

Akitoa salamu za Serikali kwenye ibada ya Pasaka iliyoandaliwa na Jumuiya ya Kikiristo Tanzania (CCT) na kufanyika kitaifa mkoani Manyara, wenyeji wakiwa ni Kanisa la Mungu Tanzania (KLMT).

"Watu ambao wanakaidi kunawa mikono kwenye maeneo ya kutolea huduma kama masoko na minada tutaanza kuwachukulia hatua za kisheria, maana wanakwamisha jitihada za kudhibiti corona," alisema Kitundu.

Alisema wapo watu wanaogoma kunawa mikono yao kama ambavyo wataalamu wanashauri, lakini watu wengine wakiambiwa wanagoma hasa mnadani.

"Sherehe ikiwezekana zisogezwe mbele ili kuepuka corona, kwa kuwa sherehe siyo rahisi kuzidhibiti kama misiba, ambayo inafanyika mchana, hiyo ni rahisi," alieleza. Naye, Askofu Mkuu wa Kanisa la Mungu Tanzania (KLMT), Eliya Dahhi, aliwataka waumini kuendelea kuiombea nchi kwa ajili ya maambukizi.

Naye, Mwakilishi wa Jumuiya ya kikiristo Tanzania (CCT), Mchungaji John Kamoyo, aliwataka waumini kunawa mikono wanapoingia kanisani na wanapotoka ili wasije wakapeleka virusi vya corona kwenye familia zao.

**Imeandikwa na Francis Godwin (IRINGA), Neema Sawaka (KAHAMA), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Jaliwason Jasson, (BABATI).**

HABARI KITAIFA

# Mahubiri Dodoma yatawala ugonjwa wa corona

**Na Waandishi wetu,**
DODOMA

IBADA za Sikukuu ya Pasaka Mkoa wa Dodoma, jana zilitawaliwa na nasaha za ugonjwa homa kali ya mapafu (Covid-19), huku Watanzania wakihimizwa kumrudia Mungu kwa kuwa ndiye anayejua dawa ya ugonjwa huo.

Mbali na hilo, waumini wanaoumwa mafua, wameshauriwa kubaki majumbani na kutokwenda kanisani ili kujiepusha kupata virusi vya ugonjwa huo.

Akihubiri katika Ibada ya Pasaka katika Kanisa Kuu la Anglikana Dayosisi ya Kati, Askofu Dickson Chilongani, aliwataka kuchukua tahadhari kubwa kujilinda kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu.

"Mbadili mienendo ya maisha, lakini tusali sana Mungu atupe ufumbuzi wa kutatua janga hili, tuzuie misongamano isiyo ya lazima mkae majumbani na familia zenu," alisema.

Alikemea unyanyapaa kwa watu ambao wamepata maambukizi au kuhisiwa, huku akisema wanahitaji kupewa faraja na si kunyanyapaliwa.

"Ugonjwa huu siyo dhambi, yeyote anaweza kuupata kama ilivyo kwa maambukizi mengine ya magonjwa, badala ya kuwanyanyapaa tutumie muda mwingi kumuomba Mungu ili ugonjwa huo usiambukize,"alisema.

Askofu huyo alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuruhusu Watanzania kumuomba Mungu kwenye nyumba za Ibada kwa kuwa ndiyo sehemu pekee inayoweza kuuondoa ugonjwa huo.

Kanisa Kuu Katoliki la Mtakatifu Paulo wa Msalaba, limeshauri waumini ambao wanaumwa mafua wakati huu wa ugonjwa wa corona kutokwenda kanisani siku za ibada.

Katika matangazo yaliyotolewa kanisani baada ya ibada ya pili ya Pasaka inayoendeshwa kwa lugha ya Kingereza iliyoongozwa na Father Erasto Kamugisha, mtoa matangazo alisema kuwa, waumini wanaoumwa mafua hawatakiwi kuhudhuria ibada ikiwa ni sehemu ya kuchukua tahadhari ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Ibada hiyo uendeshwaji wake ulikuwa wa tofauti na kama ilivyokuwa katika Pasaka za miaka ya nyuma, ikiwamo kufutwa kwa matumizi ya maji ya baraka ambayo yalikuwa yakitumika wakati wa kuingia na kutoka katika ibada.

Hata hivyo, Katika kanisa hilo, waumini wote waliohudhuria ibada hiyo hakuna aliyevaa barakoa kama ambavyo serikali ilishauri kutokana na ugonjwa huo kuambukiza kwa hewa.

Katika hatua nyingine, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Beatus Kinyaiya, akihubiri katika Misa ya kwanza, aliwahimiza wananchi kijikinga na ugonjwa wa corona, huku akiwataka vijana kuacha kudharau ugonjwa huo.

Aidha, alisema Kanisa limetenga muda kwa ajili ya sala ya kuombea ugonjwa huo.

Aliwataka waumini kila waingiapo kanisani kunawa mikono na kukaa mbalimbali tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema bila maombi ni vigumu kumshinda shetani ambaye anawatesa kupitia ugonjwa huo, huku akiwaasa kukwepa mikusanyiko.

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya

Dodoma, Amos Kinyunyu, aliwataka Watanzania kutii maagizo ya serikali kukabiliana na corona.

Aliwataka watu kutoogopa wanapopata matatizo mbalimbali kwenye maisha yao badala yake kumtegemea Mungu kwa kuwa ndiye mwenye uwezo wa kukabiliana na matatizo hayo.

"Kila kinachokuja angalia mwambie Mungu hii ni saizi yako, ikija corona sema Mungu hii ni saizi yako, namshukuru Mungu kwa kuwa Rais anajua hilo... alipoona corona imeingia akasema Mungu saizi yake ni corona, sisi tukimbilie kanisani tumuombe Mungu ndio saizi yake, na atatenda," alisema.

Kinyunyu alisema hata Yesu alifanya hivyo, alipopata mateso mengi aliinua macho yake na kumwambia Mungu mikononi mwake anaiweka roho yake na alishinda.

Aidha, alisema kuwa, ni wajibu wa kila mtu kutekeleza masharti yaliyowekwa na serikali katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Imeandikwa na Peter Mkwavila, Paul Mabeja na Renatha Msungu.

## Zitto: Ukusanyaji mapato unasuasua

**Na Maulid Mmbaga**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha (ACT- Wazalendo), Zitto Kabwe, amesema kuwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imeonyesha ukusanyaji wa mapato usioridhisha.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki katika ofisi za chama hicho, alisema ripoti hiyo imebainisha uwapo wa mporomoko wa ukusanyaji wa kodi na kupelekea kushindwa kutimiza bajeti iliyopitishwa na Bunge.

"Kupitia ripoti ya bajeti ya fedha ya Mwaka 2016-2017, Serikali ilipanga kukusanya Sh. trilion 29.5, lakini ilikusanya Sh. trilioni 25.3 na kushindwa kufikia lengo la makusanyo kwa asilimia 14.33," alisema na kuongeza:

"Ripoti ya bajeti ya fedha ya mwaka 2017-2018, jumla ya Sh. trilioni 31.7 zilitarajiwa kukusanywa, lakini zilizokusanywa ni Sh. trilioni 27.7, hivyo kutofikia lengo la makusanyo kwa asilimia 12.66."

"Bajeti ya tatu ya mwaka 2018-19, jumla ya Sh.trilioni 32.5 zilitarajiwa kukusanywa, lakini kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, zilikusanywa Sh.trilioni 25.8, hivyo kutofikia lengo kwa asilimia 21," alisema Zitto.

Kwa mujibu wa Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, kutokana na taarifa hizo, Tanzania inashika nafasi ya mwisho katika Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC).




Kiongozi wa watalii wa Hifadhi ya Taifa ya ya Kisiwa cha Saanane, Aloyce Man'gee, akiita wanafunzi wa Shule Sekondari ya Paul Boman iliyopo jijini Mwanza, kwa lengo la kuwakusanya ili waingie kutalii na kujifunza elimu ya uhifadhi katika hifadhi hiyo, makundi ya wanafunzi hufanya safari ya kutembelea hifadhi hiyo kama watalii wa ndani. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## Askofu Sosthenes: Hofu itawaondoa kuliko tatizo

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wametahadharishwa kuondoa hofu wakati huu dunia ikipambana na maambukizi dhidi ya ugonjwa wa Covid -19 unaosababishwa na virusi vya corona, kwa kuwa inaweza kuondoa maisha ya watu wengi kuliko tatizo lenyewe.

Askofu Jackson Sosthenes wa Kanisa Anglikana Dar es Salaam, alitoa tahadhari hiyo katika ibada ya Pasaka, Kanisa la Anglikana Kristo Mfalme Kinondoni, jana.

"Tusiruhusu hofu ikatutawala na kushindwa kumtegemea Mungu. Wakati mwingine hofu inaweza kukuondoa kuliko tatizo lenyewe," alisema Askofu Sosthenes.

Aliwakumbusha waumini wa dini hiyo na wananchi kwa ujumla kuwa corona ipo nchini, lakini Mungu yupo na atawavusha watu wake katika janga hilo.

Alisema, anaipongeza serikali kwa kujali wananchi wake kwa kuamua kutowataka watu kujifungia kama hatua iliyochukuliwa na baadhi ya nchi zingine duniani kwa kuwa inatambua maisha lazima yaendelee.

Askofu Sosthenes alisema sio kwamba serikali haioni hatari au haithamini maisha ya watu wake, lakini watu wanapojifungia ndani inaweza kuleta tatizo kubwa zaidi.

Alisema Rais John Magufuli amewarudisha wananchi wake katika matumaini ya kuwa maisha lazima yaendelee kwa kutambua athari inayoweza kutokea iwapo watu wataambiwa wajifungie ndani.

"Tumemuelewa na tunamshukuru, tuko tayari na tunatambua jitihada za serikali na maagizo ya kujikinga na corona," alisisitiza Askofu Sosthenes.

Aliwataka Watanzania waendelee kumshukuru Mungu naye aendelee kuwapigania kuondokana na janga hilo ambalo kwa watu kuamua kujifungia kwa hofu ya kwenda nyumba za ibada, hawana uhakika wa usalama wao hata huko walipo.

"Hata huko wanakojifungia pengine si salama kama kwenye nyumba hizo wanazoziogopa," alisisitiza.

Alisema cha muhimu ni kufuata maagizo yanayotolewa na wataalamu wa afya na serikali ya jinsi ya kujikinga na virusi hivyo na kuongeza kuwa nyumba nyingi za ibada zimejitahidi kuweka vifaa vya kutosha vya kusafisha mikono na waumini kuachiana nafasi kwenye nyumba hizo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MCA/63**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya NYALIKUNGU Wilaya ya MASWA**

**Shauri la madai No. 7/2020**

**MDAI.................................... HAPPINESS D/O MATHEW**

**DHIDI YA**

**MDAIWA....................................DOTTO S/O MAYENGA**

**KWA: DOTTO S/O MAYENGA – WA MAJENGO "A" MASWA**

Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili ujibu dai la Talaka wewe ukiwa ni mdaiwa katika shauri tajwa.

**UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya Jtatu tarehe 20/04/2020 saa 2:30 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri liweze kusikilizwa. Usikose kuhudhuria.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 09/04/2020

Hakimu Mahakama ya Mwanzo
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

215698402

# CAG afichua utata posho Naibu Waziri Ofisi ya Rais

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini utata katika malipo ya posho alizolipwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipokuwa ziarani.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu iliyopita, CAG Charles Kichere, anasema alibaini utata huo alipofanya ukaguzi maalum kuhusu matumizi ya Sh. milioni nane yaliyofanyika kwenye Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha kuanzia Julai Mosi, 2019 hadi Novemba 4, 2019.

Anasema ukaguzi wake ulibaini Sh. milioni 5.38 zilitumiwa vibaya na ofisa mmoja kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM), kupitia udanganyifu wa kuharibika kwa gari la Naibu Waziri na posho zaidi kwa makamishna ambao walikuwa katika ziara maalum kwenye mikoa ya Simiyu na Mwanza.

"Pia, nilibaini kuwa Sh. 35,508,000 (milioni 35.508) zilizotumiwa na Naibu Waziri kwenye ziara hiyo, hazikuwa na nyaraka toshelezi. Hivyo, nilishindwa kubaini ukweli kwamba kiasi hicho kilitumika.

"Vilevile, nilibaini mafuta yenye thamani ya Sh. 4,048,000 (Sh. milioni 4.048) hayakuingizwa kwenye vitabu vya safari na matumizi ya mafuta. Hivyo, nilishindwa kuthibitisha usahihi wa mafuta yaliyotumika.

"Mbali na hayo, niligundua masurufu ya Sh. 4,300,000 (milioni 4.3) yaliyochukuliwa na ofisa mmoja kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM), hayakurejeshwa wakati wa ukaguzi wangu," anabainisha.

Vilevile, CAG anasema alibaini kuwa mmoja ya maofisa wa ofisi hiyo alihujumu kiasi cha Sh. 1,000,000 (milioni moja) kwa ajili ya ununuzi wa vipeperushi ambavyo hakuvinunua.

Katika ripoti yake hiyo, CAG anapendekeza mifumo ya udhibiti ya ndani ya ofisi hiyo iboreshwe ili kupunguza hatari za udanganyifu na matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Pamoja na hayo, ninapendekeza hatua za kisheria na kinidhamu kuchukuliwa kwa maofisa wote ambao walihusika kwenye udanganyifu uliokwapua fedha za walipakodi," CAG anashauri.



Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo (kushoto), akimkabidhi Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Meru, Gurisha Mfanga, moja ya ndoo kati ya 120 na chupa 124 za sabuni alizotoa kwa chama hicho, ili wazigawe kwenye matawi yao kwa ajili ya kusaidia wananchi watakase mikono yao wanapoingia kwenye ofisi hizo kujikinga na virusi vya corona. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## TMA yatahadharisha mvua kubwa yaja

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema kuwa mvua kubwa na yenye madhara makubwa itanyesha katika mikoa sita nchini kuanzia jana hadi Aprili 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kuhusu matarajio ya hali mbaya ya hewa kwa siku tano, ilionyesha kuwa upo uwezekano mkubwa wa kutokea madhara makubwa.

Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Morogoro, Kaskazini mwa mkoa wa Lindi, Tanga, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kiwango cha athari zinazoweza kutokea ni kubwa, huku ikitoa tahadhari ya upepo mkali kwa baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Aidha, ilibainisha athari zinazoweza kutokea kuwa baadhi ya makazi ya watu yatazungukwa na maji, ucheleweshwaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Nyingine ni kuzama kwa baadhi ya vyombo vya usafiri majini pamoja na kuathirika kwa shughuli za uvuvi na usafirishaji.

Kuanzia juzi, mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ilipata mvua ndefu ambayo ilinyesha taratibu, na hadi jana jioni ilikuwa ikiendelea kunyesha na kusababisha barabara nyingi kujaa maji, hivyo kuwa kero kwa watu wengi.

# 'Waume wa watu' kikwazo wajawazito kwenda kliniki

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MPANGO wa mjamzito kuhudhuria kliniki na mwenza wake unashindwa kufanikiwa mkoani hapa, kutokana na baadhi ya wanawake kupewa ujauzito na waume za watu na kuogopa kuongozana nao kwa kuhofia kusababisha migogoro katika jamii.

Akielezea kuhusu jambo hilo, Mratibu wa afya ya uzazi na mtoto mkoani hapa, Ernest Teyumwete, alisema kuwa wanaendelea na jitihada za kuhakikisha asilimia za ushiriki katika kliniki ya baba mama na mtoto zinaongezeka kwa kuwa wameweka mikakati ya kuongeza utoaji wa elimu hiyo ili kutatua changamoto zinazokwamisha.

Teyumwete alisema kumekuwapo na makundi ya wanawake ambao hawahudhurii kliniki na wenza wao kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito kutoka kwa waume wa watu na kundi la wasichana wadogo waliopewa ujauzito na wanaume wasio tayari kuwajibika au kufahamika na jamii hivyo kuogopa kuongozana nao.

"Baadhi yao wanapohojiwa na wahudumu wa afya wanaeleza wamepewa ujauzito na waume wasio wao, hivyo hawako tayari kuongozana nao, japo katika ujazaji wa taarifa za masuala ya uzazi hakuna mahali penye maelekezo ya kujaza aina hiyo ya taarifa kwa hiyo sisi kama mkoa hatuna takwimu zake japo tatizo ni kubwa," alisema.

Teyumwete alisema sababu hizo zinafanya kundi hilo kuchelewa kuhudhulia kliniki kwa kuwa wengine wanakwenda kwa mara ya kwanza mimba ikiwa na umri wa miezi sita hadi minane na kuongeza uwezekano wa kupata matatizo wakati wa kujifungua.

Mkoa wa Kigoma awali ulikuwa na ushiriki mdogo wa chini ya asilimia 20 ya kinababa wanaowasindikiza wenza wao kliniki, lakini baada ya mikakati ya utoaji elimu ya umuhimu wa kundi hilo kuhusika katika afya ya uzazi imeongezeka kwa mwaka 2018 asilimia 56 hadi 79 kwa mwaka 2019.

Mwanamke ambaye hakutaka jina lake liandikiwe gazetini, alisema alipewa ujauzito kabla ya ndoa akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu na mwanaume aliyempa ujauzito alikuwa mkoa tofauti, hivyo hadi kujifungua hakuweza kuhudhuria kliniki na mwenza wake na pia kutokana na kupata ujauzito huo bila kutarajia kwa mara ya kwanza alihudhuria kliniki mimba ikiwa na miezi sita.

"Namshukuru Mungu nilijifungua salama japo kama ningeendelea kuchelewa kufika kliniki hali ingekuwa mbaya kwa sababu ujauzito ule ulinisumbua sana," alisema.

## HABARI KITAIFA

### Wamachinga waboreshewa masoko kwa mil. 200/-

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SHIRIKA la Misaada ya Maendeleo la Uingereza (DFID), Ubalozi wa Ireland nchini, kwa kushirikiana na Shirika la kutetea haki za wanawake na wasichana la Kivulini, wametenga zaidi ya Sh.milioni 200 kwa ajili ya kuboresha masoko ya Kiloleli wilayani Ilemela na Mirongo wilayani Nyamagana mkoani Mwanza.

Hatua hiyo imechukuliwa kufuatia wafanyabiashara wengi wa Mkoa wa Mwanza kufanyia shughuli zao katika mazingira hatarishi kutokana kukosa maeneo rasmi.

Maboresho hayo yatafanya masoko hayo kuwa na uwezo wa kutumiwa na wafanyabiashara wengi kwa wakati mmoja.

Akizungumza wakati wa ziara ya kujionea mwenendo wa ujenzi wa masoko hayo, Mkurugenzi wa shirika la Kivulini, Yassin Ally, alisema kukamilika kwa masoko hayo, yatakayokuwa na uwezo wa kubeba wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga zaidi ya 1,000, kikiwemo chumba cha kunyonyeshea watoto pamoja na kituo cha kisasa cha daladala, na kwamba kutasaidia kutatua changamoto ya wafanyabiashara hao ambao wamekuwa wakifanyia shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi.

Alisema ujenzi huo unatarajia kukamilika Aprili 30, hivyo aliwataka wafanyabiashara wadogo kubadili mitazamo na kuachana na biashara za holela katika kuelekea katika Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati.

Naye Mwenyekiti wa soko la Kiloleli, Modest Simfukwe, alisema kuboreshwa kwa masoko hayo kutachangia kupunguza msongamano wa wafanyabiashara wanaofanya biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi.

"Wale wote waliopo barabarani soko likikamilika watapewa elimu na watatoka mahali pasipo halali na kwenda panapotakiwa...unalishukuru shirika la Kivulini kwa sababu nchini hamna soko ambalo limetenga mahali pa kunyonyeshea watoto, hakika ili likikamilika litakua ni soko la mfano," alisema Simfukwe.

# RC awaamuru wazee wenye magonjwa sugu kukaa ndani

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, amewataka wananchi wa mkoa huo, ambao wanaishi na wazee na wale wenye magonjwa sugu kuwaepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima katika kipindi hiki cha ugonjwa wa (COVID-19).

Mbali na watu hao, pia amewasihi wazazi wenye watoto wadogo kutowapeleka kwenye mikusanyiko mikubwa ili kuwaepusha na ugonjwa huo.

Mtaka ametoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na viongozi wa dini na waumini wa madhebu ya Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu John Bariadi, Kanisa la Kiinjiri la Kirutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Tumaini Bariadi na African Inlanda Church Tanzania (AICT) Bariadi wakati wa ibada ya Pasaka.

Alisema makundi hayo yanatajwa kuwa ndiyo yanaathirika zaidi na ugonjwa huo, na kupoteza maisha kwa wingi, kutokana na kinga zao kutokuwa imara kama ilivyo kwa watu wengine

Aliwaambia waumini hao kuhakikisha wanawazuia au kutowapeleka watu wenye hali hizo kwenye mikusanyiko kwa kuwa ugonjwa huo bado upo nchini. "Tuwaepushe sana wazee wetu na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, watoto na wale wenye kisukari, shinikizo la damu, pumu, ugonjwa wa moyo na unene uliopitiliza nao tuwaepushe," alisema Mtaka.

"Makundi haya yakishambuliwa na corona wanapoteza haraka maisha, tafadhali naomba wakae nyumbani wakati huu, hata kwenye hii Pasaka wasitoke ndani, ugonjwa huu ni hatari," alisema Mtaka.

Pia aliwataka wakazi wa mkoa huo kuzingatia kanuni zote za usafi ambazo zimekuwa zikitolewa na watalaamu wa afya, ikiwamo kuhakikisha wananawa mikono yao kila mara na kutochukulia mzaha kwenye ugonjwa huo.

" Nimeona hapa Kanisa Katoliki, mfumo wa kukaa uko vizuri, nimeona watu wanakaa mbalimbali...lakini nimeona tatizo bado lipo katika kushiriki chakula cha bwana na kutoa sadaka, watu wanakaribiana sana, hii ni hatari," alisema Mtaka.

Naye Mchungaji Amos Ndaki wa AICT, aliwataka waumini wake mbali na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huo, lazima wamuombe sana Mungu.

Mchungaji Ndaki alisema katika kipindi hiki, lazima Wakristo waungane katika kumuomba Mungu kuepusha janga hili ambalo limeendelea kupoteza maisha ya watu duniani.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF sasa imulike maboresho viwanja mapumziko corona

**IJUMAA** wiki hii mashabiki, klabu, wadau wa michezo na Watazania, kwa ujumla wanatarajia kujua hatma ya kuendelea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara na michezo yote nchini ama la.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba Ijumaa itakuwa siku ya mwisho ya kumalizika kipindi cha mwezi mmoja ambacho serikali ilitangaza zuio la kufanyika shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kote nchini.

Serikali ilifikia hatua hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), ambavyo kwa wakati huo tayari kulikuwa na mgonjwa mmoja ambaye alipata maambukizi, huku Shirikisho la Afya duniani (WHO), likitangaza kuwa janga la kimataifa.

Hata hivyo, hali imezidi kuwa mbaya zaidi tofauti na awali kutokana na maambulizi ya virusi vya corona kuongezeka na kufikia wagonjwa 32, watano kati yao wakipona na watatu kufariki dunia hadi sasa. Takwimu kidunia zinatisha zaidi kwani hadi kufikia jana mchana jumla ya watu 109,654 walikuwa wameshapoteza maisha huku waliokwishapata maambukizi wakiwa 1,790,234 na waliotibiwa na kupona wakiwa 409,420.

Kutokana na hali hiyo, kila mtu anapaswa kuchukua tahadhari kwa kufuata kanuni na maelekezo ya kujikinga yanayotolewa na wataalamu hususan madaktari na wizara yenye dhamana ya afya nchini. Hata hivyo, kwa namna hali ilivyo kwa sasa, hakuna uhakika kama Ijumaa serikali itaruhusu kurejea kwa michezo nchini, kwani tunachokitarajia ni kuona zuio hilo likirefushwa zaidi. Lakini pia hata kama serikali itaruruhusu michezo kuendelea, bado tunatarajia kuona Shirikisho la Soka nchini (TFF) kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB), ikiongeza si chini ya wiki mbili ili kuwawezesha wachezaji kufanya mazoezi ya pamoja katika klabu zao baada ya kutengana kwa kipindi cha mwezi mzima.

Na kwa hali hiyo, wote tunafahamu ubovu wa viwanja nchini na jinsi ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa na makocha wote kuwa vimekuwa chanzo cha matokeo mabaya na wachezaji kupata majeraha ya mara kwa mara.

Hivyo, Nipashe tumeshangazwa na ukimya mkubwa wa TPLB katika kipindi hiki cha kusimama kwa michezo nchini kwa mwezi mmoja, ambacho tulitarajia ingekitumia kwa kupaza sauti kufanyiwa maboresho hususan katika eneo la kuchezea 'pitch'.


Tunatambua kipindi hiki mvua zinanyesha karibu kila kona nchini, lakini pia hakuna mazoezi ya jumla yanayofanyika katika viwanja mbalimbali ambayo yanaweza kuwa kikwazo kwa nyasi kumea vizuri. Kwa mantiki hiyo, nguvu kazi inayohitajika kwa sasa katika kuviweka viwanja vya soka nchini kwenye ubora unaostahili si kubwa sana, hivyo ni wakati wa TPLB kupaza sauti kwa wahusika ili kutumia kipindi hiki kuviboresha.

Ligi itakaporejea tunatarajia kuona nyasi zinazosapoti mpira kutembea uwanjani kama inavyotakiwa, lakini pia hatutarajii kuona maeneo ya kuzunguka eneo la kucheza ndani ya uwanja kukiwa na nyasi ndefu mithili ya zile za kuezekea nyumba.

Lakini pia itakuwa jambo la kushangaza kama baada ya ligi kuanza ndipo TPLB itaibuka na kuanza kuvifungia viwanja ambavyo havina ubora katika eneo la kuchezea wakati kulikuwa na kipindi cha mwezi mzima wa kutoa msisitizo wa maboresho hayo. Tunatambua wamiliki wa viwanja vingi vya michezo nchini si watu wa michezo (havimilikiwi na klabu za soka), hivyo pasipo TFF na TPLB kutoa msisitizo wa uboreshwaji na kuvifuatilia mara kwa mara, haviwezi kuwa katika ubora stahiki ndiyo maana tunalitaka shirikisho hilo kupaza sauti na kuvimulika mara kwa mara.

Lengo letu ni kuona TFF inatanguliza mbele afya za wachezaji kwanza kwa kuhakikisha wanacheza soka sehemu salama na mashabiki wa soka wakipata burudani tosha inayoendana na viingilio wanavyolipa ili kushuhudia mechi iwe mubashara uwanjani ama kwa njia ya luninga na hilo litatimia endapo uboreshwaji wa viwanja utafanyika katika kipindi hiki cha mapumziko ya corona.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji kambini hawalipwi, je, na corona hii nyumbani?

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** dunia ikipitia kipindi kigumu cha mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), huku ligi nyingi duniani zikiwa zimesimama, kuna maswali ambayo baadhi ya mashabiki wa soka nchini wamekuwa wakijiuliza.

Moja ni kuwa, hivi kweli baadhi ya timu zitakuwa na uwezo wa kulipa mishahara wachezaji? Kama hata huko Ulaya kuna baadhi ya klabu zimelazimika kuongea na wachezaji kuwakata mishahara kwa asilimia 20, nchini Tanzania itakuwaje?

Inawezekana kabisa klabu kadhaa zikiwamo Simba, Yanga, Azam, KMC, JKT Tanzania, Ruvu Shooting, Polisi Tanzania, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, Prisons na hata Namungo FC zikaweza kuwalipa mishahara wachezaji wao licha ya kwamba kwa muda wote huu hawajacheza mpira, wala klabu hazijaingiza chochote, lakini kwa sababu ni taasisi zinazojimudu.

Hata hivyo, hali inaweza kuwa tete kwa baadhi ya klabu kama Biashara United, Mbao FC, Alliance FC, Ndanda FC, Singida United na zingine ambazo kwa asilimia kubwa zinajiendesha kwa michango ya wahisani, wananchi na mapato kidogo ya mlangoni.

Klabu hizi inawezekana kwa sasa zinapitia kwenye kipindi kigumu mno kwani shughuli zote za soka zimesimama, lakini zinatakiwa kuendelea kuwalipa mishahara wachezaji wao ambao wapo nyumbani na familia zao.

Ukizichunguza sana klabu hizi utagundua kuwa wachezaji wao mara nyingi huishi kwa posho zinazopatikana zikisafiri na kwenda kucheza mechi, huku mishahara ikiwa kando.

Wachezaji wa timu hizi wanaweza kukaa hata miezi miwili ama mitatu bila mshahara, lakini wanaishi kwa posho zinazopatikana baada ya mechi, unajiuliza kwa sasa ambapo hakuna mechi zozote wanaishije?

Wachezaji wa baadhi ya timu hasa za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza wako kwenye wakati mgumu mno, kwani kwa sasa wapo majumbani na familia zao, lakini wanahitaji pesa kwa ajili ya kujikimu.

Tena kwa sababu wako karibu na familia, wakati mwingine pesa hutumika na kuhitajika zaidi kuliko hata wakati wao wako kambini na timu zao.

Kama tumekuwa tukisikia kesi za mara kwa mara baadhi ya klabu kutolipa wachezaji mishahara kwa wakati, wakati mwingine hadi miezi mitatu, tena wachezaji wakiwa kambini kwa ajili ya kucheza mechi, inakuwaje kipindi hiki ambacho hawako karibu na viongozi wa klabu?

Hivi kweli viongozi wa klabu hizi ndiyo wamebadilika ghafla kiasi hiki na kuwalipa mishahara au pesa ya kujikimu wachezaji kipindi hiki cha corona?

Je, siyo ndiyo kipindi ambacho hata baadhi ya viongozi wa klabu watakuwa na kisingizio kuwa hatukuwalipa wachezaji pesa zao kwa sababu hatukuingiza kitu chochote kutokana na janga la corona?

Kama hakutakuwa na mchezaji wa kulalamika kuwa hajapata pesa za kujikimu akiwa nyumbani, basi binafsi nitawapongeza viongozi wa klabu na kuona kweli sasa soka letu linaingia kwenye hatua nyingine nzuri.

Lakini uzoefu wa soka la Bongo unaonyesha kuwa hata kabla ya corona, bado kuna wachezaji walikuwa wakizidai klabu zao mishahara zaidi ya kuishi kwa posho tu.

Nina wasiwasi kunaweza kuibuka malalamiko kwa baadhi ya wachezaji kuwa wametelekezwa na viongozi wao na kuishi kwa dhiki na familia zao nyumbani.

Kwa mbali nimeshaanza kuona baadhi ya wachezaji wakianza kulalamika njaa, kutokana na kusimama kwa michezo, hivyo naona kinachofuata hapo ni kuwalalamikia viongozi wao.

Viongozi wao nao wanaweza kujitetea, lakini yeyote yule anayegombea uongozi anapaswa kujua moja ya magumu ambayo kiongozi anatakiwa apambane nayo ni hayo. Ni kama baba nyumbani anaweza kuwa hana kitu siku hiyo, lakini anafanya kila njia nyumbani familia yake ikapate chakula.

Huu ni wakati wa kila upande kutumia zaidi busara, kwa wachezaji kuwaonea huruma viongozi wao, lakini viongozi nao kuhakikisha wachezaji wao wanapata pesa za kujikimu majumbani mwao.

Kumbuka kuwa makocha wamewapa maagizo maalum wachezaji kwa ajili ya kufanya mazoezi, hivyo mchezaji hawezi kufanya mazoezi na njaa.

# CAG abaini tatizo Chadema na CCM

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika rekodi za vyama vya siasa nchini, kikiwamo chama tawala ,Chama Cha Mapinduzi (CCM) na chama kikuu cha upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu iliyopita, CAG Charles Kichere, anasema ukaguzi wake kuhusu rekodi za CCM ulibaini chama hicho kinamiliki viwanja 5,660 Tanzania Bara na Zanzibar.

Hata hivyo, CAG katika ripoti yake kuhusu ukaguzi wa hesabu za serikali kuu, anabainisha kuwa kati ya viwanja hivyo, 5,261 havina hatimiliki.

"Pia, nilibaini kuwa Jumuiya ya Wazazi ya CCM ilimfukuza mpangaji wake iliyempangisha kwenye mojawapo ya vyumba vyake kwa njia isiyokuwa halali; na ililipa jumla ya Sh. 60,000,000 kama fidia ya kumwondoa mpangaji huyo bila ya kufuata taratibu," anasema.

Vilevile, CAG anasema alibaini Shirika la Uchumi na Kilimo la Dar es Salaam (SUKIDAR), CCM ilitia saini makubaliano na kampuni ya Kikorea ya kuanzisha kampuni ya huduma ya tiba.

"Hata hivyo, niligundua kuwa hakuna mkurugenzi kutoka CCM aliyeteuliwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni iliyoundwa tofauti na masharti ya makubaliano," anabainisha.

CAG Kichere anapendekeza CCM ipitie upya sera zake za uwekezaji zilizopo, ili kukidhi mazingira ya biashara ya sasa, na kuanzisha kamati makini ya kusimamia miradi yake ya ubia.

MIL. 205/- CHADEMA

Katika ripoti yake hiyo, CAG pia anasema alikagua rekodi za Chadema na kugundua chama hicho kilitumia jumla ya Sh. 205,419,100 (milioni 205.419) bila ya idhini kutoka kwa Halmashauri Kuu ya chama.

"Pia, mapitio yangu yalionyesha Sh. 534,844,248 zilikusanywa na vyama vya siasa tisa. Hata hivyo, kiasi kilichopokewa hakikuwasilishwa kwenye akaunti za benki za vyama husika.

"Kwa kuongezea, nilibaini vyama vya siasa tisa vimetayarisha taarifa zao za kifedha bila kutamka mfumo uliotumika kuandaa taarifa za fedha. Pia, nilibaini Sh. 2,132,906,798 (bilioni 2.133) zilitumiwa na vyama vya siasa 11 bila ya kuwa na nyaraka toshelezi.

"Pia, niligundua vyama vya siasa vinne havikuandaa rejista ya wanachama. Mbali na hayo, nilibaini vyama vya siasa vinane kati ya 19 vilivyokaguliwa, havikuandaa taarifa za usuluhushi wa kibenki wa kila mwezi.

"Pia, ukaguzi wangu ulibaini vyama vya siasa vinne havikuandaa rejista ya mali. Vilevile, ukaguzi ulishindwa kubaini uwapo wa mali zilizoorodheshwa kwenye daftari la mali la UPDP.

"Kwa kuongezea, nilibaini vyama vya DP, CCK na Chaumma havikuwasilisha mali zinazomiliki kwa Msajili wa Vyama vya Siasa," CAG anafafanua.

**ATAKA CUF ICHUNGUZWE**

Katika ripoti yake hiyo, CAG Kichere pia amegusia utumiaji mbaya wa ruzuku za serikali kwenye Chama cha Wananchi (CUF), akipendekeza mifumo ya udhibiti ya ndani ya chama hicho iboreshwe ili kupunguza hatari za udanganyifu na matumizi mabaya ya fedha za mwanachama.

"Kadhalika, uchunguzi unapaswa kuanzishwa ili kupata ukweli wa matumizi ya jumla ya Sh. 416,000,000 yaliyotolewa kimashaka kwenye akaunti za benki za CUF.

"Ninapendekeza vyama vyote vya siasa kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia mfumo wa kimataifa wa uandaaji hesabu za umma (IPSAS), kama ilivyoelekezwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Pamoja na hayo, napendekeza pia vyama vya siasa kuandaa na kuhifadhi rejista za mali na wanachama, na kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi ili kuzuia hatari ya fedha za chama kutolewa kwa njia zenye shaka na viongozi wasiokuwa waaminifu," CAG anashauri.



Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya, wakiwa wamebeba karanga za kuchemsha wakitafuta wateja katika eneo la Sokoine mwishoni mwa wiki, huku mmoja wao akiwa amebeba mtoto mgongoni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sigara za magendo za mil. 275/- zakamatwa

**Na Ambrose Wantaigwa,** MUSOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeendesha msako na kukamata shehena ya sigara zilizokuwa zikivushwa kwa njia ya magendo katika mpaka wa Sirari kutoka nchi jirani.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mara, Wallace Mnkande, alisema maofisa wake wakiwa doria mwishoni mwa wiki katika mpaka huo, walikamata shehena hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 275 zikiwa zinaingizwa nchini kinyemela kupitia njia zisizo rasmi.

Alisema sigara hizo aina ya 'Supermatch' hazikuwa na nembo yoyote ya kibiashara kuonesha asili yake, ingawa alisema bidhaa zenye jina kama hilo mara nyingi huzalishwa katika nchi mbili jirani.

"Kama sigara hizo zingekuwa halali na kufanikiwa kupita katika njia rasmi, zingeweza kulipiwa ushuru kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 50, hivyo kuipatia Serikali mapato," alisema Mnkande.

Alisema njia iliyotumika ni kuchanganya na magunia ya pumba kwa lengo la kuficha ukweli, na kwamba shehena hiyo ilikuwa imepakiwa katika gari namba T 789 DKR, mali ya Esther Rhobi.

Alimtaja mtuhumiwa ambaye anadhaniwa kumiliki mzigo huo kuwa ni Ibrahim Marwa, na kwamba uchunguzi unaendelea na ukikamilika hatua stahiki zitachukuliwa.

Aliwaonya wafanyabishara katika wilaya za mpakani husussan wanaojaribu kuvusha shehena za mizigo isiyolipiwa ushuru na wakati mwingine isiyo na ubora na kuua soko la ndani.

# Mvuvi afa maji akivua

**Na Said Hamdani,** LINDI

MVUVI na mkazi wa Kata ya Rutamba, Halmashauri ya Lindi/ Mtama, Hamisi Issa Mpunga (35), amekufa maji alipokuwa anavua samaki aina ya kambale.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoani Lindi, alieleza kuwa mwili wa Mpunga umegunduliwa Aprili 8, mwaka huu na watu waliokuwa wamekwenda kwenye bwawa hilo saa 4:15 asubuhi.

Mashuhuda wa mwili wa mvuvi huyo, wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, wamedai kwamba mpunga aliondoka nyumbani kwao kwa ajili ya kuendelea na shughuli zake za uvuvi na kukutwa na mauti hayo.

"Huyu ndugu asubuhi aliaga familia yake kuwa anakwenda kwenye lile bwawa kuvua samaki, lakini hakurejea tena nyumbani," alieleza Sefu Juma.

Mashuhuda hao, Ally Said na Idrisa Yusufu, walisema kwamba mwili wa Mpunga ulikutwa ukielea na watu waliokuwa wakienda kwenye bwawa hilo kufanya shughuli zao za uvuvi, kilimo na mambo mengine.

Pia, walieleza baada ya kuukuta mwili huo ukielea juu ya maji ya bwawa hilo, walitoa taarifa kwa viongozi wa Serikali za kijiji husika, Kata na Polisi, ambapo walifika wakiwa wameongozana na mtaalamu wa afya kwa uchunguzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoani Lindi, Foka Dinya, alithibitisha mvuvi kufariki dunia kutokana na kuzama maji kwenye bwawa hilo na kueleza kuwa mwili wa mvuvi huyo ulipofanyiwa uchunguzi haukukutwa na jeraha hata moja.

Dinya alisema kwamba kwa mujibu wa maelezo ya mtaalamu wa afya aliyeufanyia uchunguzi mwili huo, kifo cha mvuvi huyo kilisababishwa na kukosa hewa wakati amezama ndani ya maji.

# Nyavu haramu za bil. 1.5/- zilivyokamatwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ameagiza kuundwa kwa kamati maalumu itakayojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya uvuvi, kwa ajili ya kuchunguza tukio la kukamatwa kwa nyavu haramu zenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.5 .

Nyavu hizo zilikamatwa eneo la Nyasaka Centre wilayani Ilemela zikiwa zimeifadhiwa kwenye nyumba ya mama mmoja kwa ajili ya kusafirishwa kwenda maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa. Zilikamatwa baada ya doria iliyofanywa na kikosi cha doria uvuvi haramu Kanda ya Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mongella alitoa maelekezo hayo baada ya kufika katika Kituo cha Polisi Nyakato jijini Mwanza akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ili kujionea nyavu hizo haramu aina ya timba na makila, kufuatia taarifa za mtuhumiwa huyo kuomba kuachiwa huru kwa kuwa yuko tayari kulipa faini ya Sh. milioni 300.

Mtuhumiwa huyo ni mfanyabiashara wa mkoani Mwanza, aliyekamatwa Aprili 4, 2020 wilayani Rorya mkoani Mara.

Alisema kuwa wasiwasi wake ni maofisa uvuvi inajitoa mhanga sana kufuatilia uvuvi haramu, isipokuwa changamoto ni wanaopambana nao kuwa watu wenye nguvu.

Alisema kama kungekuwapo utaratibu mzuri hasa wa kutoza faini, kusingekuwapo shehena kubwa ya nyavu zilizokamatwa.Kwa mujibu wa Mongella, utaratibu wa faini unaweza kuwa mwarobaini wa wanaotumia nyavu hizo kwenye uvuvi haramu. Kwa upande wake, Ofisa Uvuvi Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi, Boniface Shatila, alisema shehena ya nyavu hizo zipatazo robota 447 wamezikamata kwenye nyumba iliyopo Nyansaka Center zikiwa zimefungiwa kwenye chumba bila mhusika kuwapo hadi walipomkamatia wilayani.

"Nyavu hizi tulizikamata baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema, tuliungana na wenzetu Jeshi la Polisi tukaelekea eneo la tukio tukiwa na msiri wetu tukaanza kumtafuta mhusika wa nyumba hiyo atufungulie, lakini bahati mbaya hakuwapo, mwenye nyumba alikuwapo ila chumba kile kilikuwa cha mpangaji ambaye hakuwapo," alisema Shatila.

Naye Kaimu Mfawidhi Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Mwanza, Jacqumina Ntundu, alisema walifanya taratibu za kumkamata mtuhumiwa kule Rorya, na walimkamata usiku kisha kesho yake kupelekwa mkoani Mwanza.

Alisema alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kuwa ni Wakili Fidelix, ambaye aliumuomba waonane, na kuwa walipozungumza mtuhumiwa alikiri kwamba nyavu walizozikamata ni haramu, ila aliomba asaidiwe alipe faini.



Wananchi wa Iringa mjini, wakiwa wamebeba mwili wa Raymond Mdota (46) mkazi Magubike wilaya ya Iringa, aliyedaiwa kuchinjwa na watu wasiojulikana usiku wa Ijumaa Kuu, nje ya klabu cha pombe za kienyeji Kijiweni akiwa kwenye huduma za kueneza injili. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Akutwa ameuawa kwa kuchinjwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MTU mmoja ameuawa kinyama kwa kuchinjwa shingo na mwili wake kutupwa kwenye shamba la mahindi, wakati akifanya mahubiri ya injili kwenye kilabu cha pombe za kienyeji, siku ya Ijumaa Kuu eneo la Kijiweni, kata ya Kwakilosa, Manispaa ya Iringa.

Mtu huyo ametambulika kwa jina la Raymond Mdota (46).

Mashuhuda wa tukio hilo waliiambia Nipashe kuwa, tukio hilo lilitokea Ijumaa usiku nje ya chumba kimoja cha klabu cha pombe za kienyeji.

Walisema kabla ya mauaji hayo, Mdota ambaye ni mmoja kati ya walimu wastaafu, alifika katika eneo hilo akiwa na redio yake kubwa aliyokuwa akiikokota huku ikiwa inapiga nyimbo za dini za maombolezo ya Yesu Kristo na kuanza kuzunguka chumba kimoja hadi kingine.

"Alifika hapa muda kama saa mbili usiku akiwa na redio yake kubwa akipiga nyimbo za dini kwa sauti kubwa huku akicheza kwa furaha na kuwasisitiza watu kuachana na dhambi na kumgeukia Mungu, tulimfurahia sana hasa ukizingatia ilikuwa ni Ijumaa kuu ya mateso ya Yesu, muda ulipozidi kusogea, alianza kupiga nyimbo za muziki wa kidunia na kuanza kutangaza siasa na kujitangaza kwenda kugombea ubunge wa jimbo la Kalenga," alidai mmoja kati ya mashuhuda ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Alisema wakati akihubiri injili alikuwa ameshika rozari mkononi na baadaye alipokuwa akitangaza siasa alishika skafu yenye rangi ya bendera ya taifa na kusisitiza kuwa yeye ndiye mbunge mpya wa Kalenga, bila kutaja kupitia chama gani na kuwanunulia watu pombe huku akicheza muziki.

Hata hivyo, alisema wakati muda wa kufunga klabu ulipofika waliondoka na kumwacha na watu wachache.

Johari Ngeng'ena, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kijiweni, alisema mauaji hayo ni ya kwanza kutokea kwa mwaka huu.

Beth Mdeta, muuzaji wa pombe kwenye klabu hiyo alisema alifunga mapema na kumuacha Mdota akiwa nje ya maeneo ya klabu hicho.

"Mimi nilipigiwa simu asubuhi na majirani zangu wakinieleza kuwa nje ya chumba changu kuna mauaji yamefanyika maana kuna damu nyingi na baadhi ya vitu kama mabaki ya nguo yakiwa yametelekezwa nje ya eneo lenye damu," alisema.

Mwili wa marehemu huyo ulikutwa ukiwa umechinjwa shingo na kitu chenye ncha kali huku viatu pamoja na redio yake vikiwa vimeporwa na wauaji na mkononi akiwa ameshikilia rozari yake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo majira ya saa 10:20 alfajiri na jeshi la polisi linaendelea kuwasaka watuhumiwa wa mauaji hayo.

## Waziri Zungu aingilia kati mgogoro hoteli za baharini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amewataka wataalamu wa mazingira, kufanya tathmini ya mazingira katika maeneo ya bahari kupata dawa ya madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara katika eneo la bahari lenye mgogoro kati ya Motison wanaomiliki Hoteli ya Whitesand, wakituhumiwa na wamiliki wa Hoteli ya Wellworth Kunduchi kujenga ukuta baharini na kusababisha maji kujaa hotelini kwao. Akizungumza katika eneo hilo akiwa ameambatana na watendaji kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), waziri huyo aliwataka kuwa wavumilivu na kusubiri wataalamu wa sayansi ya bahari wafanyie kazi na kutoa majibu wiki ijayo.

Waziri Zungu pia aliwataka wananchi kuacha tabia ya kukata miti ovyo kwa kuwa ndiyo sababu kubwa ya maji ya bahari kujaa isivyo kawaida na kuingia katika maeneo yao.

"Leo tunatazama mgogoro wa watu wawili, kesho tutakuwa na watu watano au sita, tupeni muda, nimekuja hapa na Mkurugenzi wa NEMC na wataalamu wake kutazama na dawa ya tatizo tulilonalo, kwa hiyo wiki ijayo tutawaita na tutawaambia tulichofanya kuhakikisha kila mtu ana amani, ndiyo kazi ya serikali," aliahidi.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwataka wawekezaji wote kufanya tathmni ya athari za mazingira (EIA) ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima. Alisema binadamu wanaishi kwa kutegemeana kwenye mazingira na ndiyo maana NEMC haitoi cheti hadi ifanyike tathmnini kubaini madhara yanayoweza kutokea kwa wananchi kupitia uwekezaji unaofanyika.

"Natoa rai kwa wawekezaji wote, wawe wa viwanda ama hoteli katika fukwe zetu, kufanya tathmini na kupitia tathmini hiyo tutapata maoni kutoka kwa watu wanaokuzunguka kujua je, uwekezaji wako unawaathiri vipi? Na kama kuna athari ndogo tunajua namna ya kuzitatua ili kuepusha migogoro," alisema.

Akitoa maoni yake kuhusu tatizo hilo, Mtaalamu wa Sayansi ya Bahari, Rose Mtui alisema suluhisho ni kuotesha mikoko ambayo inalinda fukwe zisibomoke kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Alisema uchimbaji mchanga holela katika kingo za miti na uvuvi haramu unachangia tatizo la kimazingira katika fukwe za bahari kwa kuwa unaharibu matumbawe ambayo yakiharibika mawimbi ya bahari hugonga moja kwa moja na kwa kasi fukwe na hivyo maji kujaa kupita kiasi.

# Vyavu haramu za bil. 1.5/- zilivyokamatwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ameagiza kuundwa kwa kamati maalumu itakayojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya uvuvi, kwa ajili ya kuchunguza tukio la kukamatwa kwa nyavu haramu zenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.5 .

Nyavu hizo zilikamatwa eneo la Nyasaka Centre wilayani Ilemela zikiwa zimeifadhiwa kwenye nyumba ya mama mmoja kwa ajili ya kusafirishwa kwenda maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa. Zilikamatwa baada ya doria iliyofanywa na kikosi cha doria uvuvi haramu Kanda ya Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mongella alitoa maelekezo hayo baada ya kufika katika Kituo cha Polisi Nyakato jijini Mwanza akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ili kujionea nyavu hizo haramu aina ya timba na makila, kufuatia taarifa za mtuhumiwa huyo kuomba kuachiwa huru kwa kuwa yuko tayari kulipa faini ya Sh. milioni 300.

Mtuhumiwa huyo ni mfanyabiashara wa mkoani Mwanza, aliyekamatwa Aprili 4, 2020 wilayani Rorya mkoani Mara.

Alisema kuwa wasiwasi wake ni maofisa uvuvi inajitoa mhanga sana kufuatilia uvuvi haramu, isipokuwa changamoto ni wanaopambana nao kuwa watu wenye nguvu.

Alisema kama kungekuwapo utaratibu mzuri hasa wa kutoza faini, kusingekuwapo shehena kubwa ya nyavu zilizokamatwa.Kwa mujibu wa Mongella, utaratibu wa faini unaweza kuwa mwarobaini wa wanaotumia nyavu hizo kwenye uvuvi haramu. Kwa upande wake, Ofisa Uvuvi Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi, Boniface Shatila, alisema shehena ya nyavu hizo zipatazo robota 447 wamezikamata kwenye nyumba iliyopo Nyansaka Center zikiwa zimefungiwa kwenye chumba bila mhusika kuwapo hadi walipomkamatia wilayani.

"Nyavu hizi tulizikamata baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema, tuliungana na wenzetu Jeshi la Polisi tukaelekea eneo la tukio tukiwa na msiri wetu tukaanza kumtafuta mhusika wa nyumba hiyo atufungulie, lakini bahati mbaya hakuwapo, mwenye nyumba alikuwapo ila chumba kile kilikuwa cha mpangaji ambaye hakuwapo," alisema Shatila.

Naye Kaimu Mfawidhi Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Mwanza, Jacqumina Ntundu, alisema walifanya taratibu za kumkamata mtuhumiwa kule Rorya, na walimkamata usiku kisha kesho yake kupelekwa mkoani Mwanza.

Alisema alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kuwa ni Wakili Fidelix, ambaye aliumuomba waonane, na kuwa walipozungumza mtuhumiwa alikiri kwamba nyavu walizozikamata ni haramu, ila aliomba asaidiwe alipe faini.



Wananchi wa Iringa mjini, wakiwa wamebeba mwili wa Raymond Mdota (46) mkazi Magubike wilaya ya Iringa, aliyedaiwa kuchinjwa na watu wasiojulikana usiku wa Ijumaa Kuu, nje ya klabu cha pombe za kienyeji Kijiweni akiwa kwenye huduma za kueneza injili. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Akutwa ameuawa kwa kuchinjwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MTU mmoja ameuawa kinyama kwa kuchinjwa shingo na mwili wake kutupwa kwenye shamba la mahindi, wakati akifanya mahubiri ya injili kwenye kilabu cha pombe za kienyeji, siku ya Ijumaa Kuu eneo la Kijiweni, kata ya Kwakilosa, Manispaa ya Iringa.

Mtu huyo ametambulika kwa jina la Raymond Mdota (46).

Mashuhuda wa tukio hilo waliiambia Nipashe kuwa, tukio hilo lilitokea Ijumaa usiku nje ya chumba kimoja cha klabu cha pombe za kienyeji.

Walisema kabla ya mauaji hayo, Mdota ambaye ni mmoja kati ya walimu wastaafu, alifika katika eneo hilo akiwa na redio yake kubwa aliyokuwa akiikokota huku ikiwa inapiga nyimbo za dini za maombolezo ya Yesu Kristo na kuanza kuzunguka chumba kimoja hadi kingine.

"Alifika hapa muda kama saa mbili usiku akiwa na redio yake kubwa akipiga nyimbo za dini kwa sauti kubwa huku akicheza kwa furaha na kuwasisitiza watu kuachana na dhambi na kumgeukia Mungu, tulimfurahia sana hasa ukizingatia ilikuwa ni Ijumaa kuu ya mateso ya Yesu, muda ulipozidi kusogea, alianza kupiga nyimbo za muziki wa kidunia na kuanza kutangaza siasa na kujitangaza kwenda kugombea ubunge wa jimbo la Kalenga," alidai mmoja kati ya mashuhuda ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Alisema wakati akihubiri injili alikuwa ameshika rozari mkononi na baadaye alipokuwa akitangaza siasa alishika skafu yenye rangi ya bendera ya taifa na kusisitiza kuwa yeye ndiye mbunge mpya wa Kalenga, bila kutaja kupitia chama gani na kuwanunulia watu pombe huku akicheza muziki.

Hata hivyo, alisema wakati muda wa kufunga klabu ulipofika waliondoka na kumwacha na watu wachache.

Johari Ngeng'ena, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kijiweni, alisema mauaji hayo ni ya kwanza kutokea kwa mwaka huu.

Beth Mdeta, muuzaji wa pombe kwenye klabu hiyo alisema alifunga mapema na kumuacha Mdota akiwa nje ya maeneo ya klabu hicho.

"Mimi nilipigiwa simu asubuhi na majirani zangu wakinieleza kuwa nje ya chumba changu kuna mauaji yamefanyika maana kuna damu nyingi na baadhi ya vitu kama mabaki ya nguo yakiwa yametelekezwa nje ya eneo lenye damu," alisema.

Mwili wa marehemu huyo ulikutwa ukiwa umechinjwa shingo na kitu chenye ncha kali huku viatu pamoja na redio yake vikiwa vimeporwa na wauaji na mkononi akiwa ameshikilia rozari yake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo majira ya saa 10:20 alfajiri na jeshi la polisi linaendelea kuwasaka watuhumiwa wa mauaji hayo.

## Waziri Zungu aingilia kati mgogoro hoteli za baharini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amewataka wataalamu wa mazingira, kufanya tathmini ya mazingira katika maeneo ya bahari kupata dawa ya madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara katika eneo la bahari lenye mgogoro kati ya Motison wanaomiliki Hoteli ya Whitesand, wakituhumiwa na wamiliki wa Hoteli ya Wellworth Kunduchi kujenga ukuta baharini na kusababisha maji kujaa hotelini kwao. Akizungumza katika eneo hilo akiwa ameambatana na watendaji kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), waziri huyo aliwataka kuwa wavumilivu na kusubiri wataalamu wa sayansi ya bahari wafanyie kazi na kutoa majibu wiki ijayo.

Waziri Zungu pia aliwataka wananchi kuacha tabia ya kukata miti ovyo kwa kuwa ndiyo sababu kubwa ya maji ya bahari kujaa isivyo kawaida na kuingia katika maeneo yao.

"Leo tunatazama mgogoro wa watu wawili, kesho tutakuwa na watu watano au sita, tupeni muda, nimekuja hapa na Mkurugenzi wa NEMC na wataalamu wake kutazama na dawa ya tatizo tulilonalo, kwa hiyo wiki ijayo tutawaita na tutawaambia tulichofanya kuhakikisha kila mtu ana amani, ndiyo kazi ya serikali," aliahidi.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwataka wawekezaji wote kufanya tathmni ya athari za mazingira (EIA) ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima. Alisema binadamu wanaishi kwa kutegemeana kwenye mazingira na ndiyo maana NEMC haitoi cheti hadi ifanyike tathmnini kubaini madhara yanayoweza kutokea kwa wananchi kupitia uwekezaji unaofanyika.

"Natoa rai kwa wawekezaji wote, wawe wa viwanda ama hoteli katika fukwe zetu, kufanya tathmini na kupitia tathmini hiyo tutapata maoni kutoka kwa watu wanaokuzunguka kujua je, uwekezaji wako unawaathiri vipi? Na kama kuna athari ndogo tunajua namna ya kuzitatua ili kuepusha migogoro," alisema.

Akitoa maoni yake kuhusu tatizo hilo, Mtaalamu wa Sayansi ya Bahari, Rose Mtui alisema suluhisho ni kuotesha mikoko ambayo inalinda fukwe zisibomoke kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Alisema uchimbaji mchanga holela katika kingo za miti na uvuvi haramu unachangia tatizo la kimazingira katika fukwe za bahari kwa kuwa unaharibu matumbawe ambayo yakiharibika mawimbi ya bahari hugonga moja kwa moja na kwa kasi fukwe na hivyo maji kujaa kupita kiasi.

# Vijana 29 wakamatwa kusababisha msongamano

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

UONGOZI wa Soko la Mawenzi, Manispaa ya Morogoro, umewakamata vijana 29 wanaodaiwa kuzurura katika soko hilo na kufanya msongamano unaotishia afya zao katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covic-19.

Katibu wa soko hilo, Nemes Mkiwa, alisema operesheni hiyo imefanywa na uongozi wa soko jana asubuhi kwa kushirikiana na mgambo wa Manispaa hiyo.

Alisema wamelazimika kuwaruhusu vijana 23 baada ya kuwatambua kuwa walishawahi kuomba kufanya kazi ndogo ndogo sokoni hapo na kutakiwa kukamilisha utaratibu wa usajili ili watambulike.

Mkiwa alisema vijana sita wamepewa kazi ya kusafisha soko kwa siku nzima kwa mujibu wa sheria za soko na kutakiwa kutoonekana tena maeneo ya soko hilo. Alisema vijana hao wakionekana sokoni hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Alisema wamelazimika kufanya operesheni hiyo kutokana na kusajili vijana 35 ambao wanafanya biashara ndogo ndogo ikiwamo kuuza mifuko, maji na kubeba mizigo ya wanunuzi.

Mmoja wa waliokamatwa, Nonga Hamisi (19), alisema amekamatwa na askari hao akidaiwa kutokuwa na jezi ya kufanya biashara hiyo sokoni.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akinawa mikono na vitakasa mikono, nje ya jengo la ofisi yake. Muro ameendelea kutoa elimu juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona. **PICHA WOINDE SHIZZA**

# Macha awacharukia waliopewa viwanja bure na kuviuza

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amesema wafanyabiashara waliogawiwa viwanja 600 bure na kuviuza au kukodisha kwa Sh. 500,000 huku wakirudi kufanya shughuli vichochoroni watachukuliwa hatua.

Wafanyabiashara hao waliopewa viwanja hivyo ni wanaofanya weldingi, wachonga masofa na wauza mbao ambao walitakiwa kuondoka katikati ya mji na kwenda pembezoni kuepusha msongamano.

Macha aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuwa viwanja hivyo waligawiwa bure ili wao waweze kulipia hati na baadhi waliotekeleza na kufanikiwa kupata hati hizo kukopea kwenye taasisi za fedha.

Alisema, wapo wafanyabiashara walichukua maeneo hayo na kuuzia watu wengine kwa Sh. 300,000 na wengine wakikodisha kwa Sh. 500,000 huku wao wakienda kufanyia shughuli zao vichochoroni.

"Sasa nitaanza kuwashughulikia kwa kufanya operesheni na waliouza au kukodisha kwa gharama kubwa watajuta na wale wanaoleta bidhaa zao kuonyesha shoo watatuonyesha leseni zao wanatengenezea wapi bidhaa, hatukatazi kuwa na shoo ya bidhaa mjini bali watuonyeshe wanatengenezea wapi ili tuweze kubaini waliouza viwanja,"alisema Macha.

Mwenyekiti wa halmashauri ya Kahama, mji Abeli Shija, alikiri wafanyabiashara kugaiwa viwanja mwaka 2017, lakini hakuna uhakika kama waliviuza au kukodisha. "Kama wanafanya kuuza maeneo ni kosa, kitu ambacho hatukukiangalia kutunga sheria ndogo itakayombana mtu atakayebainika kuuza atachukuliwa hatua gani," alisema Shija.

Alisema wafanyabiashara wanaoleta shoo ya bidhaa zao mjini ikiwa wana meneo yao ya kufanyia shughuli hakuna shida, lakini wasifanyie vichochoroni mahali ambapo pamezuiliwa na halmashauri kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Kahama, Anderson Msumba, alisema hivi sasa wanaanza kufanya tathmini ili kubaini maeneo ambayo waliwagawia kushindwa kuyaendeleza na kuwapatia wafanyabiashara wenye nia.

# DC aagiza vifaa kinga kuwekwa mpakani

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Msafiri Mtemi, ameagiza vifaa kinga dhidi ya virusi vya corona vilivyotolewa na mgodi wa dhahabu wa North Mara, kuwekwa katika njia zote rasmi za kuingia na kutoka katika mpaka wa Tanzania na Kenya ili kuzuia maambukizi mapya.

Pia ameelekeza vifaa hivyo kuwekwa katika maeneo ya mikusanyiko ya watu ikiwa pamoja na makanisani, misikitini na masoko kama tahadhari kwa ajili ya kupima wananchi wote ambao wataonyesha dalili za awali za maambukizi hayo.

Alisema wakati akipokea msaada huo, wilaya hiyo ya mpakani ilitenga maeneo ya karantini kuweka wasafiri na wageni wote walioingia nchini kupitia mpaka wa Sirari kutoka maeneo hatarishi ya maambukizi ulimwenguni kwa gharama zao kulingana na maagizo ya serikali kupitia Wizara ya Afya.

"Tumeagiza pia wasimamizi wa kikosi kazi cha afya kilichoundwa kuratibu mapambano ya corona maeneo haya pia kuhakikisha wanapeleka baadhi ya vifaa muhimu kama vile vipima joto katika maeneo ya wachimbaji wadogo wilayani hapa ambako pia kuna misongamano ya watu," alisema Msafiri.

Katika hatua nyingine alionya wakazi wilayani hapa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki kuelekea Sikukuu za Pasaka tofauti na ilivyozoeleka na kuepuka misongamano isiyo ya lazima, kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni katika maji yanayotiririka kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mgodi huo unaomilikiwa na Kampuni ya Barrick uliopo katika mji mdogo wa Nyamongo, wilayani hapa ulikabidhi vifaa kinga vyenye thamani ya Sh. milioni 37 katika mamlaka za wilaya na pia utasambazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya corona.

Vifaa hivyo ni pamoja na matangi 120 ya kunawa mikono yenye ujazo wa lita 200 kila moja, chupa za vitakasa mikono (sanitizers), viatu na suti maalumu za wahudumu wa afya zinazotarajiwa kutumika kuhudumia washukiwa wa maambukizi ya virusi hivyo.

Kwa upande wake, Meneja wa usalama na afya wa mgodi huo, Nicholas Mboya, alisema kampuni hiyo ilikabidhi msaada huo kwa ajili ya kulinda jamii zinazozunguka maeneo ya uwekezaji ili kuunga mkono juhudi za serikali kukabiliana na maambukizi mapya ya corona.

# Waomba Kigoma ilindwe mipakani

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WADAU kutoka taasisi mbalimbali mkoani hapa wametakiwa kushirikiana na serikali kuongeza nguvu utoaji wa elimu ya ugonjwa wa virusi vya corona (Covid- 19), kutokana na mkoa huo kuwa na mipaka mikubwa ya wazi inayopakana na nchi za Burundi na Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, ambazo zina maambukizi ya ugonjwa huo.

Mratibu wa Shirika la Msalaba Mwekundu Mkoa wa Kigoma, Khalid Seleman, alitoa wito huo wiki iliyipita ukiwa mwendelezo wa kuelimisha wananchi kwa kutumia matangazo ya sauti mitaani, ugawaji wa mabango na vipeperushi vya elimu kuhusu ugonjwa huo.

"Bado tunahitaji nguvu za kutosha katika kufikisha hili jambo, wananchi wanachukulia mzaha suala hili, tunazunguka katika maeneo mbalimbali tunashuhudia zile kanuni za usafi hazifuatwi," alisema.

Aprili 6, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emannuel Maganga, aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama mkoani humo kuwakamata watu ambao hawazingatii maagizo ya kujikinga na jumla ya watu 16 walikamatwa na kufikishwa polisi.

"Hao 16 walikuwa wa kuanzia, walilala kituoni na baadaye wakatoka, wengine watakao bainika ni moja kwa moja mahakamani tutawafungulia mashtaka," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko la Katonga, Manispaa ya Kigoma Ujiji, Mohamed Ntejeko, aliomba watoa elimu kujikita zaidi utoaji machapisho ili kuwezesha elimu kufika kwa ufasaha kwa wananchi na kusaidia wao kwa wao kuelekezana.

"Uwezekano wa kila mwananchi kupata maelekezo ya moja kwa moja kutoka kwa daktari ni ngumu hivyo tunaiomba serikali itoe machapisho mengi ya elimu ya namna ya kujikinga na corona," alisema.

Naye Mratibu wa magonjwa ya mlipuko ya Covid-19 na Ebola Mkoa wa Kigoma kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu, Mahamudu Msonga, alisema zoezi hilo wameshirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (Unicef).

Msonga alisema, wanakusudia kutoa elimu hiyo kwa wilaya zote sita katika mkoa huo na hadi sasa wameshagawa mabango ya machapisho 800, na vipeperushi 3,200 kati ya 12,000 walivyonavyo na wataangalia pia uhalisia wa mahitaji ili ikiwezekana waongeze kuandaa machapisho mengine zaidi.

# Mgogoro shamba wamwibua mwekezaji

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WANANCHI wa kijiji cha Mhenda, Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 14 katika shamba la Mhenda lenye ukubwa wa hekari 623 ambalo linadaiwa kuchukuliwa na mwekezaji.

Wakizungumza katika mkutano wa kijiji hicho, walisema shughuli za kimaendeleo kijijini hapo zimesimama kutokana na mgogoro huo kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa kijiji hicho ni wakulima.

Wakazi hao walisema wameanza kulima katika shamba hilo tangu mwaka 1975, lakini mwaka 2006 mwekezaji huyo akaibuka na kudai kuwa eneo hilo ni la kwakwe jambo ambalo lilizua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

"Nimekuja kijiji hiki mimi tangu mwaka 1974 nilikuta wakati pamba ndio inachipukia mpaka watu wakachuma, alikuja hadi Mwalimu Nyerere hapa baada ya kumalizika pamba tukakabidhiwa kulima na sisi ndio tulianza," alisema Salma Jumbe, mkazi wa Kijiji Mhenda.

Baadhi ya wananchi walipandwa na jazba na kutaka kwenda kuvamia shamba hilo ili waliendeleze baada ya kukaa muda mrefu bila kutumiwa na mwekezaji huyo. "Huyu mwekezaji hajawahi kulima hata mara moja tangu alipotupora shamba letu, leo anasema anashamba Mhenda kitu mbacho si cha kweli hata kidogo, sasa kilichobaki sasa hivi wote wenye maeneo yetu tuende tukawatoe watu wake na vitu vyao," alisema Fabiani Mapunda.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Franco Stando, aliwataka wananchi hao kuacha kujichukilia sheria mkononi, kwa kuwa kufanya hivyo kutawanyima haki yao na kuwataka kuungana kufuata sheria katika kudai shamba hilo.

"Tukienda kufanya fujo adhma yetu haiwezi kukamilika kutashindwa kuunda hoja tukienda kwa mkuu wa mkoa, tuendelee kufuata sheria kwasababu nyaraka zetu zinaonyesha mwaka 1985 wakati mwalimu Nyerere anaaga aliruhusu wananchi tuendelee kulima," alisema.

Diwani wa Kata ya Mhenda, Japhet Kageuka, alifafanua kuwa baada ya kupokelewa kwa hati ya mgogoro wa shamba hilo katika ofisi ya kata hatua mbalimbali zilichukuliwa kufatilia suala hilo wakati shughuli za kijamii zikiendelea eneo hilo.

Alisema tayari suala hilo lilishafika Ofisi ya Wilaya Kilosa na kwa sasa imeshaundwa kamati kwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kufikisha madai yao ili haki iweze kutendeka na mchakato bado unaendelea.

Kwa upande wake mwekezaji huyo anayetuhumiwa kuchukua shamba hilo, Saleh Mohamed, alisema eneo hilo alirithi kutoka kwa baba yake na anamiliki kihalali kwa kuwa hati miliki zote anazo.

"Kiuhalisia lile shamba lina hati miliki liko chini ya Kamishna wa Ardhi na kuhusiana na mgorogoro umeshaamrіwa na Mahakama Kuu ya Dar es salaam, kwa hiyo mimi nimerithi kutoka kwa baba yangu ambaye alilinunua kwenye mnada wa mahakama tangu 2006," alifafanua.

Kilosa ni miongoni mwa wilaya saba za Mkoa wa Morogoro ambayo inakabiliwa na migororo ya ardhi ya mara kwa mara kufuatia baadhi ya wawekezaji kuyatelekeza mashamba hayo kwa muda mrefu.



Mohamed Mgata, mkulima wa mahindi katika kijiji cha Magulilwa mkoani Iringa, akinyunyizia dawa wa kuua wadudu hivi karibuni.
**PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# DPP azitaka benki kufuata sheria ufunguaji akaunti

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mashtaka Nchini (DPP), Biswalo Mganga, amezionya benki na watumishi wake watakaofungua akaunti bila kufuata utaratibu na sheria, zitawajibika na tuhuma za kutakatisha fedha.

Kadhalika, amesema watumishi wa benki watakao kubali kufungua akaunti zenye majina ya taasisi za serikali na zikatumika kuchota fedha za umma au kodi za serikali atakula nao sahani moja.

Kauli hiyo aliitoa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio la kutakatisha fedha kupitia majina ya Taasisi za serikali.

"Wafanyakazi wa benki muwe makini mnapofungua akaunti zenye majina ya Taasisi za Umma ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), zinazopitisha fedha nyingi bila kufuatilia uhakika kutoka mamlaka au taasisi husika, benki zitawajibika na utakatishaji fedha, sitawaacha," alionya.

Akifafanua zaidi alisema mtu binafsi alikwenda Benki ya CRDB tawi la Msasani akafungua akaunti ya kukusanya kodi kwa Sh. 150,000, lakini mfanyakazi wa benki hakushtuka wala hakupiga simu kwa Kamishna Mkuu wa TRA.

Alisema mtu huyo baada ya kufungua hiyo akaunti alisambaza barua kwa wafanyabiashara akiwaelekeza akaunti namba ya kulipia kodi na kwamba mfumo wa kutoa kontroo namba umeharibika wanapaswa kulipa kupitia akaunti hiyo.

"Machi 6, mwaka huu Mfanyabiashara mmoja alilipa serikali kodi kupitia akaunti hiyo feki Sh. milioni 27.3, mtuhumiwa alianza kutoa kidogo kidogo ndipo vyombo vya dola vikaanza kumfuatilia na kumnasa....," alisema.

Wakati huohuo, Mfanyabiashara Dioniz Kaskazi, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka sita, ikiwamo kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 27.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Nipashe
# Spotika



MAGOLIKIPA 10 BORA KATIKA HISTORIA YA EPL UK. 12 & 13



## ISIKUPITE

Yanga iliwahi kufuzu kucheza robo fainali ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika (Kwa sasa Ligi ya Mabingwa) mara mbili, mwaka 1969 na 1970 na katika hatua zote ilitolewa na Asante Kotoko ya Ghana, hata hivyo katika robo fainali ya mwaka 1969, iliondoshwa kwa njia ya kura ya shilingi, baada ya matokeo ya jumla kuwa sare ya bao 1-1.

# XAVI NA NIA YA UKOCHA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez daima atakumbukwa kama gwiji pale Barcelona. Kiungo huyu mbunifu alikuwa alama ya klabu hiyo chini ya utawala wa Pep Guardiola, na inatabiriwa kwamba atarudi pale Camp Nou kama kocha siku moja.

Kipindi chote cha uchezaji wake kwenye nafasi ya kiungo aliiongoza vema Barcelona pamoja na Andres Iniesta na Sergio Busquets ambapo kwa pamoja walitengeneza kizazi cha dhahabu.

### KUIONGOZA KATALUNYA

Wanasema kwamba maisha yanaanza ukiwa na umri wa miaka 40, lakini siku chache kabla ya kutimiza umri huo, akiwa na miaka 39, Xavi alinukuliwa akisema kwamba, hajihisi kama yupo tayari kwa kazi ya ukocha kwa timu ambayo amehusika nayo katika maisha yake yote ya soka. Kwa sasa anainoa timu ya Al-Sadd in Qatar, akiwa anatafuta nafasi ya kujiimarisha zaidi kabla ya kuiongoza miamba hiyo ya Catalunya.

Majadiliano kati ya Xavi na Barcelona yaliyofanyika Januari yalikuwa na malengo ya kumpa nafasi ya kumrithi kocha wa zamani, Ernesto Valverde. Hata hivyo, Xavi, aliamua kuikataa nafasi hiyo, akidai kwamba huo si wakati wake kuchukua nafasi hiyo. Baadaye Valverde nafasi yake ilichukuliwa na kocha wa sasa, Quique Setien.

### UAMUZI MGUMU

Ulikuwa uamuzi mgumu kwa Xavi kuufanya, na chaguo lake lingetenganisha kichwa na moyo. Hasa ikizingatiwa uzoefu wake kwenye nafasi ya ukocha. Lakini hilo linaweza kusemwa pia kuhusu Guardiola wakati alipopandishwa kutoka timu B hadi kikosi cha kwanza mwaka 2008. Yaliyobaki kwake ni historia.

Lakini kama ilivyokuwa kwa Guardiola, Xavi ni gwiji klabuni pale kutokana na mafanikio aliyoyapata wakati akicheza.

Xavi angeweza kujiona yeye mwenyewe kwa Guardiola wakati alipochukua mikoba hiyo muongo mmoja uliopita na kushuhudia kile alichokifanya licha ya kuwa na presha kubwa kutokana na kutokuwa na uzoefu wa kutosha.

Wakati wa kuinoa Barcelona mara zote itakuwa ndoto kwa mtu kama Xavi, ni jambo nzuri katika hali hiyo kutoikimbilia kazi hiyo. Kwani kama angeshindwa kutokana na uzoefu mdogo, hangeweza kupata nafasi ya pili. Angekuwa na majuto ambayo yangemuandama kwa kipindi chote cha maisha yake ya ukocha.

### MUDA NDIO KILA KITU

Lakini nafasi kama hii inakuja mara moja tu, na kama Xavi hatapata mafanikio kwa klabu nyingine wakati akiendelea kujiimarisha yeye mwenyewe kama kocha, anaweza asiitwe tena Barcelona. Xavi alifanya uamuzi wa kimahesabu Januari kwamba, atachukua kazi hiyo wakati atakapokuwa tayari, na mawazo yake yanatakiwa kuheshimiwa.

Lakini Xavi alitimiza miaka 40 baadaye Januari, na inaonekana umri huo umebadilisha mtazamo wake. Janga na virusi vya corona (COVID-19) limetikisa dunia na kila kitu kimebadilika, na Xavi alizungumza wikiendi iliyopita kuhusu nia yake ya kuchukua nafasi pale Camp Nou.

### MAADILI YA KWELI

"Nipo wazi kwamba nataka kurudi Barcelona, nina hamasa kubwa," alielezea Xavi katika mahojiano na gazeti la La Vanguardia la nchini Hispania. "Sasa najiona mwenyewe kwenye nafasi ya ukocha, nafikiri naweza kuleta vitu kwa wachezaji. Lakini lazima niweke wazi kwamba, najiona mimi mwenyewe kwenye mradi ambao ulianzia chini kabisa na mimi mwenyewe nilikuwa kwenye maamuzi."

Kauli ya Xavi ilifungua mlango mwingine, na hakuna shaka kwamba klabu itafanyia kazi kauli hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa Setien hayupo kwenye presha kubwa kama ilivyokuwa kwa Valverde kwa wakati huu, na Xavi anahisi kwamba anaweza kuendelea kujiimarisha kama kocha.

### KUKUMBATIA PRESHA

Uamuzi wa Xavi umekuja kutokana na muda wa kuteuliwa kwake. Atapata muda wa kutosha zaidi kujifunza pale Al-Sadd, na uzoefu wa kuiongoza Barcelona dimbani unaweza kuwa muhimu zaidi kwa kizazi kinachokuja ambacho kwa sasa kinajiimarisha chenyewe kwenye timu ya wakubwa.

Na sasa Xavi ana nafasi ya kupata mafanikio makubwa zaidi wakati wa uongozi wake kwenye ukocha. Matarajio ni makubwa sana pale Camp Nou, lakini anatakiwa kuikumbatia presha yake.

# MAGOLIKIPA 10 BORA KATIKA HISTORIA YA EPL

**LONDON,** England

ZAMA za Ligi Kuu ya England zimeshuhudia maendeleo kwa baadhi ya timu bora katika historia ya soka la Uingereza, huku zikiwa na mafanikio makubwa kama Manchester United, Arsenal na Liverpool. Lakini wakati timu zote hizi zikiwa zimejumuisha washambuliaji wakali, mafanikio yao yasingeweza kufikiwa bila ya kuwa na magolikipa bora.

**Makala haya yanakuchambulia magolikipa 10 bora kwenye historia ya Ligi Kuu ya England, ambao ni hawa hapa...**

### #10 JOE HART

Kiwango alichokionyesha akiwa na timu ya Taifa ya England na baadaye West Ham na Burnley, kilisababisha heshima yake kushuka, lakini wakati akiwa kwenye ubora wake, Joe Hart alikuwa kipa mwenye uwezo wa kuvutia. Zao hili la mfumo wa kulelea vipaji wa pale Shrewsbury, Hart alihamia Manchester City mwaka 2006 akiwa na umri wa miaka 19, lakini kiwango chake kilichomoza miaka mitatu baadaye.

Msimu wa 2009-10, ukamfanya apelekwe kwa mkopo Birmingham, ambapo alifurahia wakati wake na kujikuta akitajwa kwenye kikosi cha mwaka cha Ligi Kuu England. Kutoka hapo akajiimarisha yeye mwenyewe kama golikipa namba moja wa Man City, alicheza mechi 18 bila kuruhusu bao msimu wa 2010-11, akishinda tuzo ya kipa bora wa mwaka.

Baadaye akajiimarisha pia kama golikipa namba moja wa England, na Hart akashinda tuzo tatu zaidi akiwa na City. Msimu wa 2011-12 alishinda taji la Ligi Kuu akiwa na klabu hiyo, na alirudia hivyo msimu wa 2013-14.

Licha ya kuanza kushuka kiwango muda ulivyokuwa ukienda, mwaka 2015 pengine alionyesha kiwango bora zaidi kwa kipindi chake cha uchezaji kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona. Katika mchezo huo aliokoa hatari 10, pamoja na kutoa penalti ya Lionel Messi.

Tangu alivyoondoka City baada ya kuwa na kiwango duni kwenye michuano ya Euro 2016, Hart hajawa kwenye ubora wake tena.

### #9 KASPER SCHMEICHEL

Mara zote ilikuwa ni ngumu kwa Kasper Schmeichel kufuata nyayo za baba yake, Peter. Lakini golikipa huyo namba moja wa Leicester City na timu ya Taifa ya Denmark, amekuwa na kiwango cha kuvutia kwa kipindi cha muongo mmoja sasa.

Zao la akademi ya kukuza vipaji ya Manchester City, Schmeichel, alicheza kwa mkopo katika timu nyingi wakati wa ujana wake. Akianzia kule Notts County na baadaye Leeds United, lakini mafanikio yake makubwa ameyapata tangu ahamie Leicester mwaka 2011.

Alitajwa mchezaji bora wa mwaka wa timu hiyo kwenye msimu wake wa kwanza, alicheza mechi 19 bila kuruhusu bao katika msimu wa 2013-14 ambapo aliiongoza timu yake hiyo kupanda kucheza Ligi Kuu. Lakini msimu wa 2015-16 ndio bora zaidi katika maisha yake ya soka.

Msimu huo ulishuhudia Leicester wakitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu ya England. Nyota huyo wa kimataifa wa Denmark alicheza mechi 15 bila kuruhusu bao, akiokoa hatari 99 na kuruhusu mabao 36, wakati wakiwa chini ya kocha, Claudio Ranieri.

Tangu hapo Schmeichel ameendelea kujiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa magolikipa bora kwenye Ligi Kuu ya England.

### #8 JENS LEHMANN

Golikipa Mjerumani, Jens Lehmann, alichezea Arsenal kwa misimu mitano kutoka mwaka 2003 hadi 2008 na kufanya makubwa kwenye Ligi Kuu ya England. Msimu wake wa kwanza ndio kwa uhakika ulikuwa na mafanikio makubwa zaidi, alikuwa sehemu ya kikosi cha 'Washikabunduki' wa London waliocheza msimu mzima bila kupoteza mchezo.

Katika msimu huu alicheza mechi 15 bila kuruhusu bao na aliruhusu mabao 26 pekee. Msimu wa 2004-05, kulimfanya atajwe kuwa nyota wa mchezo kwenye kipute cha fainali ya Kombe la FA wakati Arsenal ikishinda kwa penalti; huku Lehmann akiokoa penalti ya Paul Scholes.

Msimu wa 2005-06, ulimshuhudia akicheza mechi 100 za Ligi Kuu ya England, na kuisaidia Arsenal kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hiyo ilikuwa historia nzuri kwa Mjerumani huyo wakati alipocheza mechi 10 bila kuruhusu bao katika mashindano yote, kabla ya kuondoka Arsenal mwaka 2008.

### #7 ALISSON BECKER

Alisson Becker alisajiliwa Liverpool akitokea Roma mwaka 2018, na kwa sasa ni mmoja wa makipa bora duniani tangu ajiunge na 'Wekundu' hao wa Anfield.

Akiwa anaitwa kwa jina la utani la 'Messi wa magolikipa', Alisson alicheza mechi 21 bila kuruhusu bao katika msimu wake wa kwanza, huku akifungwa mabao 22 kwa msimu mzima. Na hiyo ilitosha kumfanya atwae tuzo ya golikipa bora wa msimu.

Kiwango chake langoni kiliisaidia Liverpool kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Baada ya makosa ya Loris Karius kuigharimu Liverpool kwenye fainali ya mwaka 2018, Alisson alibadilisha mambo na kuwa nguzo muhimu kwa msimu wote na akiokoa hatari nane kwenye fainali waliyobeba kombe.

Katika umri wake wa miaka 27, ni wazi kwamba anaweza kutumia muongo mmoja akiwa kileleni pale Liverpool. Kwa sasa anatazamiwa kushinda taji lake la kwanza la Ligi Kuu ya England msimu huu.

### #6 DAVID DE GEA

Ni golikipa namba moja wa Manchester United, akiwasili hapo mwaka 2011. David De Gea amekuwa mmoja wa magolikipa bora kabisa kwenye Ligi Kuu. Alisajiliwa akiwa na umri wa miaka 20, alishutumiwa na wengi kwa kufanya makosa wakati wa msimu wake wa kwanza.

Tangu hapo ameimarika na kuimarika zaidi. Msimu wa 2013-14 alikuwa kwenye ubora zaidi kwa kuokoa hatari nyingi akatwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa United, huku msimu wa 2014-15 ukamfanya aingie kwenye timu bora ya mwaka. Msimu wa 2017-18 ukamfanya ashinde tuzo ya golikipa bora wa mwaka, baada ya kucheza mechi 18 bila kuruhusu bao.

Wakati wa kukumbukwa zaidi? Pengine alivyookoa hatari kwenye mchezo dhidi ya Sunderland, mwaka 2013, alisifiwa kwa kuwa kipa bora kwenye historia ya soka. Na mwaka 2017, alivunja rekodi ya Ligi Kuu kwa kuokoa hatari nyingi zaidi, akitoa 14 kwenye mchezo wa ushindi dhidi ya Arsenal.

Katika miaka ya hivi karibuni, tangu alipokuwa na kiwango kibovu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, akiwa na Hispania nchini Urusi, De Gea mwenye umri wa miaka 29, amekuwa akifanya makosa mengi ya kuruhusu mabao kizembe.

### #5 EDWIN VAN DER SAR

Wakati Peter Schmeichel alipoondoka Manchester United mwaka 1999, iliwachukua miaka kadhaa 'Mashetani Wekundu' hao kupata mrithi wake sahihi. Makipa kama Mark Bosnich, Fabian Barthez na Tim Howard walishindwa, lakini Edwin Van Der Sar alifanikiwa.

Mholanzi huyo alikuwa na umri wa miaka 34, wakati aliposajiliwa na United na akafurahia misimu minne ya nguvu na Fulham kwenye Ligi Kuu. Lakini pale Old Trafford ndipo haswa alipoonesha thamani yake.


Msimu wake wa pili United ulishuhudiwa 'Mashetani Wekundu' hao wakitwaa taji la Ligi Kuu, huku yeye akitajwa kwenye kikosi bora cha mwaka. Msimu wa 2007-08 ulikuwa bora zaidi kwake. Si tu kwamba United walitetea taji lao, lakini walishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Mdachi huyo aking'ara kwenye penalti.

Msimu wa 2008-09 ulimshuhudia akivunja rekodi ya Ligi Kuu ya England; akisaidia United kucheza mechi 11 na dakika 1032 bila kuruhusu bao.

Maisha ya Van Der Sar pale United yaliisha mwaka 2011 baada ya misimu sita. Wakati wake akiwa pale alishinda mataji saba klabuni hapo.

### #4 EDERSON

Wakati Pep Guardiola alipochukua mikoba ya kuinoa Manchester City mwaka 2016, moja ya kazi yake ya kwanza ilikuwa ni kumuondoa Joe Hart kwenye kikosi cha kwanza. Sababu zake alitaka kipa mwenye uwezo na akili ya kudaka na kuokoa, hivyo, akamsajili Claudio Bravo, raia wa Chile, ambaye hakuweza kuonyesha kiwango chake kwa kusababisha makosa mengi.



PETR CECH

Kipindi cha majira ya joto cha 2017, kilishuhudiwa City wakimsajili kipa wa Brazil, Ederson. Ederson aliisaidia City kushinda taji la Ligi Kuu, akiruhusu mabao 27. Alicheza mechi 16 bila kuruhusu bao.

Mara kwa mara amekuwa akiacha goli lake na kujifanya kama mlinzi wa ziada, na Ederson amekuwa na wastani mzuri wa pasi sahihi kwa asilimia 85. Mabao mengi ya City yameanzia kwa pasi za golikipa huyo.

Msimu wa 2018-19, alishinda taji lake la pili la Ligi Kuu pamoja na FA na EFL. Na halikuwa jambo la kushangaza kumshuhudia akitajwa kwenye kikosi cha timu bora ya mwaka.

### #3 DAVID SEAMAN

Mmoja wa magolikipa wanaoheshimiwa kwa wakati wote, David Seaman, ambaye alikuwa golikia namba moja wa Arsenal kwa misimu 13 ya kuvutia. Kwa kipindi hicho akiisaidia Arsenal kutwaa mataji tisa, yakiwamo mawili ya Ligi Kuu.

Msimu wa 1997-98 ulikuwa wake wa kwanza kutwaa taji la Ligi Kuu, lakini 1998-99 pengine ndio ulikuwa msimu bora zaidi kwake. Alicheza kila mechi kwa 'Washikabunduki' hao, akiruhusu mabao 17, wakati wakimaliza nafasi ya pili. Mwishoni mwa muongo wake mmoja mwaka 2002, hakuna golikipa mwingine aliyecheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, akicheza 130.

Seaman ndio mchezaji wa pili wa Arsenal kucheza mechi nyingi zaidi akifikisha 325.

### #2 PETR CECH

Alisajiliwa Chelsea kipindi cha majira ya joto mwaka 2004, Petr Cech alitumia misimu 11 kama golikipa namba moja pale Blues. Wakati wake akiwa pale Stamford Bridge, alishinda mataji 13, yakiwamo manne ya Ligi Kuu.

Golikipa huyu raia wa Czech msimu wake wa kwanza alicheza mechi 21 bila kuruhusu bao akishinda taji la Ligi Kuu na kushinda tuzo ya kipa bora wa mwaka, wakati akiruhusu kufungwa mabao 15 kwa msimu. Msimu wa 2005-06 ulimshuhudia akifungwa mabao 22, wakati Chelsea ikishinda tena taji la Ligi Kuu.

Msimu wa 2009-10 ulimshuhudia akishinda tuzo ya golikipa bora wa mwaka na alifikisha mechi 100 bila kuruhusu bao kwa kipindi alichocheza Chelsea, na msimu wa 2010-11, ulimshuhudia akichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa klabu.

Pengine wakati bora zaidi kwake ni msimu wa 2011-12. Kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich, aliokoa penalti katika muda wa ziada na nyingine mbili kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti na kuwasaidia 'Blues' hao kushinda taji la michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

Cech baadaye alihamia Arsenal, na ingawa hakuwa na mafanikio makubwa alishinda Kombe la FA mwaka 2017.

### #1 PETER SCHMEICHEL


Aliyekuwa kocha wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, kuna wakati alimtaja Peter Schmeichel akiwa golini huongeza pointi za ziada 15 kwa msimu mzima. Kiukweli, pengine hakukosea. Raia huyo wa Denmark alitumia misimu nane pale Old Trafford na kuisaidia timu hiyo kufikia mafanikio makubwa kwa kipindi chote alichokaa hapo.

Katika msimu wake wa kwanza klabuni hapo, ulimshuhudia akishinda taji la Ligi Kuu. Wakati wa msimu huo alicheza mechi 22 bila kuruhusu bao, na alitajwa kuwa golikipa bora wa mwaka. Kutokea pale, alikwenda kushinda mataji mengine manne ya Ligi Kuu, na mengine sita likiwamo la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1999.

Schmeichel bado anabaki kuwa golikipa bora kwenye Ligi Kuu ya England, licha ya kustaafu miaka 15 iliyopita.

## Nukuu

"Kama nguli wa Liverpool, nataka kufikia vitu vya kushangaza hapa, tuna timu bora, hatupungukiwi chochote, tuna zana zote muhimu za kushinda, kocha ambaye tunatambulika naye, kikosi cha aina nyingi ya uchezaji ambao unazalisha ushindi, uwanja na mashabiki wanaocheza sehemu yao, ningependa kuwa mmoja miongoni mwa wachezaji ambao watarudi Anfield baada ya kustaafu," **beki wa Liverpool, Virgil van Dijk.**



"Ukweli ninampenda Ney [Neymar], uchezaji wake ni wa kushangaza. Lakini anapaswa kuwa mtaalamu zaidi kama [Cristiano] Ronaldo na [Lionel] Messi, ambao wanaishi kwa soka. Ney ana maoni mengi sana ambayo yanamtia wasiwasi, nimezungumza naye hivi karibuni na kumtaka kuwa mtaalamu," **nguli wa Brazil, Zico**



"Naweza kusema Raheem Sterling; ndiye mpinzani mgumu kumkaba, anakimbia kwa kasi. Mara zote nikicheza dhidi yake nakabiliwa na changamoto kubwa mno, ndio maana nampenda," **beki wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka**





ZAMA za Ligi Kuu ya England zimeshuhudia maendeleo kwa baadhi ya timu bora katika historia ya soka la Uingereza, huku zikiwa na mafanikio makubwa kama Manchester United, Arsenal na Liverpool.

Uk. 12&13



# SABABU HAZARD KUCHEMSHA REAL

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amekuwa na wakati mgumu katika mwaka wake wa kwanza kucheza Madrid, nini kilichomfanya kiungo huyo mchezeshaji kukwama pale Real?

**Mashabiki wa Real Madrid walikuwa na furaha kubwa wakati Hazard alipoondoka Chelsea na kukubali kusaini kwa mabingwa hao mara 13 wa Ulaya Julai mwaka jana, dili ambalo lilitajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 130.**

Mchezaji mwenyewe alielezea furaha yake wakati akitambulishwa kwa mashabiki wa klabu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Hispania: "Nilikuwa na ndoto ya muda mrefu kutua hapa tangu nikiwa mtoto, mara zote nilikuwa shabiki wa Real Madrid. Nitajaribu kuwa bora duniani."

Miezi nane baadaye Hazard akazungumzia msimu wake wa kwanza pale Bernabeu na kusema: "Msimu wangu wa kwanza pale Madrid ulikuwa mbaya," alisema akinukuliwa na RTBF.

"Ulikuwa msimu wa kuzoea ligi. Natakiwa kuhukumiwa msimu wa pili. Ni suala langu kuwa kwenye kiwango kizuri mwakani."

Takwimu zake akiwa Chelsea zinaonyesha kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kuanzia mwaka 2012 hadi 2019 alicheza jumla ya mechi 245 za Ligi Kuu ya England, akifunga mabao 85 na kutoa pasi za mwisho 'asists' 54 na nafasi alizotengeneza 595 na mashuti 491.

Wakati tangu atue Real Madrid kwa msimu 2019-20 amecheza mechi 10 za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, akifunga bao moja, 'asists' moja na nafasi alizotengeneza 14 na mashuti 12.

Wakati Hazard alipojiunga na klabu hiyo kubwa duniani, alikuwa ameingia rasmi kwenye anga za Galactico, ikiwa ni miaka sita baada ya Gareth Bale kutua pale Bernabeu,

**UZITO**

Mara baada ya kutua Real Madrid, Hazard alianza kushutumiwa kwa kuongezeka uzito kupita kiasi wakati akitoka kwenye likizo ya majira ya joto.

Hata yeye mwenyewe alikubaliana na hilo. "Ni kweli," Hazard alikubali kwamba ameongezeka uzito katika mahojiano na gazeti la L'Equipe Novemba mwaka jana. "Siwezi kuficha, lakini niliongezeka uzito kwa sababu nilikuwa likizo."

Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger wakati akitoa maoni yake kuhusu kuongezeka uzito kwa Hazard alisema: "Kama unataka farasi ashindwe kwenye mbio, muongeze kilo mbili katika kilo zake 500."

**MAJERUHI**

Majeruhi nayo yamemtikisa Hazard, kwani aliumia wakati wa mazoezi kabla ya kuanza kuichezea mchezo wa kwanza Real Madrid dhidi ya Celta Vigo.

Na matokeo yake alilazimika kusubiri kuanza kucheza mechi yake ya kwanza ya ushindani Septemba na kumfanya kocha, Zinedine Zidane kulazimika kuwa mtulivu.

"Najua kwamba atapata mafanikio hapa," alisema kocha Zidane raia wa Ufaransa wakati akimsubiria Hazard kucheza mechi yake ya kwanza.

Lakini Hazard akashindwa kufunga katika mechi zake tano za kwanza katika mashindano yote na gazeti la Marca likamfananisha na Michael Owen ambaye ndiye mchezaji aliyeanza vibaya zaidi akiwa kama 'Galactico' baada ya Muingereza huyo kucheza mechi saba za mwanzo bila kufunga bao hapo Bernabeu.

"Ni kweli kwamba watu walitarajia makubwa kutoka kwangu, pia mimi mwenyewe nilitarajia makubwa," alisema Hazard, baada ya kucheza mechi hizo tano bila kufunga.

Bahati nzuri, hatimaye akafunga bao lake la kwanza wakati timu yake ikipata ushindi wa 4-2 nyumbani dhidi ya Granada Oktoba.

**HATUA MOJA MBELE, MBILI NYUMA**

"Sikuwa vizuri," alikubali Novemba. "Nilijiambia mwenyewe kuanza kucheza vizuri."

"Miezi miwili ya kwanza, haikutosha. Nilidhani naweza kufanya vizuri. Sifanyi vizuri, lakini najaribu."

Mambo yalionekana kuwa mazuri wakati alipoonyesha kiwango cha kuvutia katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Eibar baadaye mwezi huo na hata gazeti la AS likaandika katika ukursa wake wa kwanza: "Hatimaye Hazard amefika."

Kiwango chake alichokionyesha ndicho kilichokuwa kikitarajiwa na kila mmoja nchini Hispania.

Lakini wakati mashabiki wakiwa na furaha na kiwango chake, Hazard akaumia kifundo cha mguu kwenye mchezo wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain na hivyo kumfanya awe benchi wakati wa hatua ya 16-bora.

**NAMBA 7 ISIYO NA BAHATI**

Hazard alikuwa nje ya uwanja hadi Februari na akarudi kwenye mchezo dhidi ya Celta, huku mchezaji huyo akipewa heshima ya mashabiki kusimama uwanjani dakika ya 73 kwenye mchezo huo katika dimba la Bernabeu.

Siku sita baadaye, akarudi tena kwenye vyumba vya matibabu baada kuvunjika kifundo cha mguu wakati Real Madrid ikikumbana na kichapo cha 1-0 kutoka kwa Levante.

Na sasa Hazard amekosa mechi nyingi zaidi kutokana na majeruhi katika msimu wake wa kwanza hapo Real Madrid kuliko miaka yake saba aliyocheza pale Chelsea.

**MUDA WA KUZOEA LIGI**

Bila shaka, Hazard hatakuwa mchezaji wa kwanza ambaye alihitaji muda wa kuzoea mazingira ya timu mpya, nchi na ligi.

Kocha Pep Guardiola akimzungumzia Hazard alionyesha kushangazwa kwa kushindwa kufanikiwa kwa mchezaji huyo pale Madrid.

"Kama hachezi vizuri, kuna kitu kinaendelea pale Madrid kwa sababu kwa hakika kabisa yeye ni mchezaji mzuri," alisema kocha huyo wa zamani wa Barcelona.

"Kile tulichokiona England... ni mchezaji wa daraja la juu duniani. Lakini dunia nzima inajua kwamba kuna wakati mchezaji anahitaji muda wa kuzoea mazingira."

**USILOLIJUA**



MOHAMED Hussein 'Mmachinga', ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi Ligi Kuu Bara baada ya kucheka na nyavu mara 26 msimu wa 1999, rekodi ambayo imedumu kwa miaka 21 sasa. Mwaka 2006 Abdallah Juma, mchezaji wa zamani wa Mtibwa, alikaribia kuifikia rekodi ya Mmachinga, lakini akajikuta akiishia kufunga mabao 25. Msimu huu Meddie Kagere wa Simba tayari ana mabao 19 huku timu yake ikibakiza mechi 10 kabla ya ligi kumalizika, je ataivunja?



## HABARI DODOMA

# DC Chemba afunga daraja Kelema

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

MKUU wa Wilaya ya Chemba, Saimon Odunga, amelifunga daraja la Kelema Maziwani linalounganisha mikoa ya Tanga, Dodoma, Manyara na Singida, kutokana na kuhatarisha maisha kwa watumiaji.

Daraja hilo kingo zake zimesombwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha, hivyo halitakiwi kutumiwa na vyombo vya moto.

Odunga alitangaza uamuzi huo alipokuwa akizungumza na wananchi mwishoni mwa wiki katika kijiji cha Simba, Kata ya Mondo.

Hata hivyo, alisema kuwa ufungaji huo hautaathiri wanaopita kwa miguu katika daraja hilo.

Mkuu huyo alikemea vikali vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wakazi wa maeneo hayo kuendelea kulitumia daraja hilo kupitisha magari, hali inayoongeza uharibifu mkubwa zaidi.

Aliutaka uongozi wa Kijiji cha Simba kuimarisha ulinzi katika daraja hilo ili kuhakikisha halitumiki kwa shughuli zozote za usafirishaji hadi hapo daraja hilo litakapofanyiwa ukarabati.

"Kufanya hivyo kutasaidia kupunguza athari zaidi na gharama za ukarabati wa daraja hilo," alisema.

Odunga aliwataka wananchi kuwa watulivu na wenye subira kipindi ambapo wanasubiri ukarabati wa daraja hilo.

Aidha, aliwataka wananchi kutumia njia mbadala iliyoelekezwa na serikali ili kuendelea na shughuli zao za kila siku.

"Hii ni mara ya pili daraja hili kufungwa na uharibifu huu umetokana na mvua zinazonyesha na pia licha ya kuwa hatari wananchi wameendelea kulitumia daraja na kuzidisha uharibifu," alisema.



Mtoto Lolini Lucas (4) kushoto na Elisha Mwambapa (4), wakazi wa mtaa wa Itega, Kikuyu jijini Dodoma, wakitekeleza maelekezo ya serikali pamoja na wazazi wanaoishi nao, ya kunawa maji na sabuni kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya corona. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# LAAC yafunguka nidhamu matumizi ya fedha S/Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Abdallah Chikota, amesema nidhamu ya matumizi ya fedha imeimarika ndani ya miaka minne kwenye mamlaka za serikali za mitaa nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Chikota ambaye pia ni Mbunge wa Nanyamba, alisema awali mamlaka hizo zilipewa majina mengi ikiwamo mchwa kutokana na matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Nimpongeze Rais John Magufuli kwa kuwa Tamisemi iliyoko chini yake, amefanya kazi kubwa ya kuimarisha utendaji kazi, mtakumbuka awali zilipewa majina mengi mchwa kutokana na kula fedha sasa hivi kuna maboresho makubwa sana.

"Hata taarifa iliyowasilishwa hivi karibuni na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuna maboresho makubwa sana," alisema.

Alieleza kuwa katika taarifa hiyo hati zinazoridhisha kwenye mamlaka hiyo zimeongezeka kutoka asilimia 81 hadi 95 huku asilimia tano ni hati zenye mashaka na hakuna hati chafu.

"Utayarishaji wa hesabu kwenye mamlaka za serikali za mitaa umeimarika na usimamizi wa matumizi pia umeimarika kwa kiwango kikubwa ...hivi sasa kuna nidhamu kubwa sana ya matumizi ya fedha, zamani haikuwa ajabu Kamati ya LAAC inakwenda kukagua nyumba ya Mganga mkuu wa wilaya unaenda hadi site nyumba haionekani unaambiwa ulikuwa mpango," alisema.

Chikota alisema sasa hakuna hali hiyo, na kwamba hivi karibuni Kamati hiyo ilitembelea Mkoa wa Iringa na Njombe kukagua ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za wilaya na kulikuwa na miradi mizuri yenye ubora inayolingana na thamani ya fedha.

"Miradi hii imejengwa kwa mfumo wa 'force account', utaratibu huu umeokoa fedha nyingi ambazo zingepitia kwa makandarasi, wataalam wetu kuna wakati walikuwa wanaleta gharama sio halisi, kwa kweli usimamizi umeimarika kwa kiwango kikubwa, unaona kabisa mradi umejengwa na kwa viwango," alisema.

Hata hivyo, alisema bado kuna kero chache ambapo baadhi ya watendaji wanafanya kazi kwa mazoea.

"Kwa mfano, Halmashauri ya Mbogwe tulikuta Sh. milioni 400 hazipo benki na Kituo cha Afya hakipo, Songea DC wamekusanya kupitia mashine ya POS Sh.Milioni 400 lakini hapo katikati kwenda benki zimepotea hata kabla ya kwenda," alisema.

Alisema Ofisi ya Rais, Tamisemi imetafuta mwarobaini ya kudhibiti hilo ambapo imeanzisha kitengo cha usimamizi na ufuatiliaji wa fedha kwenye serikali za mitaa na mikoa ambacho kinabaini tatizo kabla ya CAG kufika.

"Changamoto ya matumizi ya fedha kwenye Halmashauri za Mkoa wa Morogoro zilibainiwa na hichi kitengo kabla ya CAG, na inasaidia kuokoa fedha, kwa ujumla kuna maboresho makubwa sana, Tamisemi chini ya Waziri Selemani Jafo hatua zinachukuliwa haraka tofauti na awali, " alisema.

# DC awatuliza watumishi mauaji ya mwalimu mkuu

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, amewasihi watumishi wa wilaya hiyo, kuwa watulivu na wavumilivu wakati serikali inaendelea kuwachukulia hatua watu waliohusika kumuua Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chilingulu, Heladius Mgaya (41).

Mwalimu Mgaya aliuawa kwa kukatwa mapanga na watu wasiojulikana usiku Aprili 6, mwaka huu, katika kijiji cha Chilingulu wilayani humo.

Munkunda alitoa kauli hiyo katika ibada fupi ya kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa Mgaya, iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo mwishoni mwa wiki.

Akizungumza katika ibada hiyo, Mkuu huyo alisema ukatili huo hautafumbiwa macho na kuwatoa hofu watumishi kuwa serikali kupitia vyombo vyake vya dola itachukua hatua stahiki kwa wahusika.

"Huu ni ukatili kama ulivyo ukatili mwingine na kamwe haukubaliki, naomba mtambue kuwa Serikali ipo kazini na wahusika watachukuliwa hatua stahiki kwani kazi hii tayari imeshaanza.

"Mimi na Mkurugenzi baada ya kupata taarifa za tukio hili, mara moja tulikwenda eneo la tukio ambapo tuliungana na viongozi ngazi ya kata, na kiukweli tunakemea matukio maovu kama haya na ninaahidi kuwa wale wote waliohusika vyombo vya dola vinaendelea na kazi na sheria itachukua mkondo wake," alisema.

Mkuu huyo aliongeza: "Hatuwezi kukubali hii hali, sumu hii iwe mwisho kwa sababu inawezekana tusipoikomesha itaendelea kututafuna sisi wote, maana yake sisi wote ni watumishi wa serikali bila kujali wewe unatumika katika eneo gani."

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Dk. Fatuma Mganga, alikemea vitendo vya kuwanyanyasa na kuwafanyia ukatili watumishi kwenye wilaya hiyo.

"Tukio hili ukilitafakari kibinadamu mioyo yetu inaguswa sana na unaona kabisa kutokea kwake ni kukosekana kwa upendo na wahusika kutokuwa na hofu ya Mungu...sisi kama serikali wajibu wetu ni kufuatilia watoto wote kwenda shule sasa hili kwa ndugu zetu wa Chilungulu wakati Mwalimu Mgaya akitekeleza hilo alionekana kuwa kero kwao," alisema.

Kadhalika, Dk. Mganga aliwaomba viongozi wa dini kubuni mbinu mpya ya kuokoa roho za watu zilizopotea kwani maumivu yanayosababishwa na watu wasio na hofu ya Mungu ni makali.

"Penye upendo hatutegemei kukuta kitu kama hiki, hii ni chuki, ndiyo maana imesababisha tukio kama hili ambalo linasononesha sana," alisema.





## Wananchi Mbeya waonyesha mwitikio mkubwa kunawa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKOA wa Mbeya, umetajwa kuwa miongoni mwa yenye mwitikio mkubwa kwa wananchi wake kunawa mikono kwa kutumia sabuni kama ilivyoagizwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wataalam wake ili kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Timu kutoka Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Msanii Mrisho Mpoto, ilifanya ziara mkoani Mbeya kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tahadhari ya ugonjwa wa Covid-19.

Aliwahamasisha wananchi kutambua umuhimu wa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara ili kuepukana na maambukizi.

Alisema Wizara ya Afya itafikia mikoa 13 ambayo iko kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya corona ikiwemo Songwe, Rukwa, Katavi, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam.

"Kampeni hii ya utoaji elimu dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 na kuhamasisha wananchi kunawa mikono ina lengo la kukabiliana na ugonjwa huo na kuifanya Tanzania kuwa salama zaidi, hili suala ni la kila Mtanzania, naomba tushirikiane," alisema Mwakitalima.

Balozi wa kampeni hiyo msanii, Mrisho Mpoto, alisema kupitia sanaa yake atawafikia wananchi wa maeneo mbalimbali na kwamba ugonjwa huo usiwagawe Watanzania badala yake uwakutanishe pamoja ili kuukabili.

Aliwaomba wadau kuunga mkono jitihada hizo za serikali katika kuutokomeza ugonjwa huo kwa kuyagusa makundi mengine ikiwamo wenye ulemavu ili kupata elimu ya kujikinga.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walieleza umuhimu wa kunawa mikono kwa majisafi na salama kwa kutumia sabuni ili kuepuka maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

# Wasioweka ndoo na sabuni faini 300,000/-

**Na Grace Mwakalinga,**

MBARALI

MKUU wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amewaagiza watendaji wa kata na vijiji kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwatoza faini ya kuanzia Sh. 50,000 hadi 300,000 wafanyabiashara na bodaboda wanaokaidi agizo la kuweka ndoo ya maji na vitakasa vya kunawa mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Mfune alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, alipokuwa akikagua maeneo mbalimbali ya kibiashara pembezoni mwa barabara kuu ya Iringa - Mbeya, eneo la Igawa, kuangalia utekelezaji wa agizo la kila maeneo ya kutolea huduma kuwa na ndoo za maji na sabuni.

Alisema suala la kunawa mikono sio ombi ni la lazima na kila eneo la kutolea huduma viwekwe vifaa, watakaokaidi biashara zao zifungwe au watozwe faini.

"Lazima tuchukue tahadhari dhidi ya ugonjwa huu wa corona, tusipuuze masharti ya kunawa mikono kila mara na kila sehemu unapoingia kupata huduma, hii itasaidia kujikinga na maambukizi, utaratibu huu lazima ufuatwe kama umeshindwa funga biashara, lakini sio kuweka rehani maisha ya wengine," alisema Mfune.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Michael Semindu, aliwasihi watumia sigara na wanywaji pombe kali kuacha tabia ya kupokezana vilevi hivyo kwa kuwa ni rahisi kupata maambukizi.

Aliwataka wanywaji wa pombe kuacha tabia ya kurundikana chumba kimoja watu wengi ili kupunguza hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa corona.

Ofisa afya wilayani humo, Said Sadick, alisema Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 inawataka wauzaji wa maduka ya dawa za binadamu, mifugo na pembejeo za kilimo kuweka vitakasa mikono, maji pamoja na sabuni ili wateja kabla na baada ya kupata huduma wanawe.




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, akipanda kwenye treni katika Karakana ya Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara), iliyopo eneo la Iyunga jijini Mbeya, alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miundombinu ya Reli hiyo ambayo ilikuwa imeharibiwa na mafuriko. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# 'Wazazi dhibitini watoto wasizurure'

**Na Grace Mwakalinga,**
MEEYA

OFISA afya wa Mkoa wa Mbeya, Mashaka Juma, amewashauri wazazi na walezi kuwadhibiti watoto wao kwa kutowaruhusu kufanya biashara maeneo ya sokoni, kucheza mpira au kuangalia sinema kwenye vibanda ili kuwakinga na maambukizi ya virusi vya corona ambavyo kwa sasa vimekuwa tishio duniani.

Aliwaambia waandishi wa habari kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo kwa kuwa ni kundi lililo kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa.

Juma aliyasema hayo juzi wakati wa semina kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya iliyokuwa na lengo la kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Alisema serikali ilifunga shule zote nchini ili kukabiliana na maambukizi ya virusi hivyo kwa watoto, lakini hali iliyopo sasa baadhi ya wazazi wanatumia mwanya huo kuwatumikisha watoto kazi za sokoni au kuwaruhusu kwenda kucheza mpira bila tahadhari yoyote.

Ni wakati sasa kwa wazazi kuacha tabia ya kupuuza mambo, huu ugonjwa ni hatari kuliko tunavyofikiria, tuchukue tahadhari tusiruhusu watoto wetu watoke nje, wabaki ndani kuna kazi nyingi za kufanya ikiwamo kujisomea," alisema Juma.

Aliwahimiza wanahabari kujenga utamaduni wa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au vitakasa mikono kila mara na kabla au baada ya kutumia vifaa vyao.

Pia, wavae barakoa wanapoenda kutafuta habari kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu.

Alisema mkoa huo umejipanga kukabiliana na ugonjwa wa Covid -19 kwa kufungua vituo mbalimbali vya kutolea huduma katika kila wilaya kwa watakaothibitika na maambukizi.

Alisema pia wataalamu wanawahimiza wafanyabiashara kutengeneza kifaa maalum cha kunawia mikono badala ya kila mmoja kushika koki ili kupunguza maambukizi.

# Sheha afukuzwa kazi kukiuka zuio la mikusanyiko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Vuai Mwinyi Mohammed, amemfukuza kazi Sheha wa shehia ya Mkokotoni, Ame Haji Ame, kwa kushindwa kutekeleza agizo la serikali la kuzuia mikusanyiko ndani ya shehia yake.

Akizungumza ofisini kwake Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema Sheha huyo ameshindwa kusimamia agizo hilo kutokana na eneo lake la Mkokotoni kuwa na nyumba inayotumika kuweka abiria wanaosafiri kwenda Tanga zaidi ya watu 50 kwa wakati mmoja jambo ambalo linaweza kusababisha maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema masheha wote walishaambiwa kusimamia maagizo yote yanayotolewa na serikali katika kupambana na kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona, lakini katika shehia hiyo ilikutwa nyumba hiyo na hali ya kuwa yeye anatambua hilo.

Alisema nafasi yake hiyo itakaimiwa na Sheha wa shehia ya Mto wa pwani, Omar Ali na tayari Mkuu wa Mkoa huyo ameifunga nyumba hiyo kutumika kwa shughuli hizo.

Katika hatua nyingine, serikali ya mkoa huo imelazimika kuwaweka ndani watu wawili wanaofanya kazi katika ofisi inayosafirisha mizigo katika Bandari ya Mkokotoni kuelekea Tanga.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazni A Unguja, Hassan Ali Kombo, alilazimika kuchukua hatua hiyo kufuatia agizo lililotolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mohamed Ahmada Salum, kuiagiza serikali ya wilaya hiyo, kuifungia ofisi hiyo kutokana kuvunja utaratibu na sheria zilizowekwa na serikali.

Awali, Naibu Waziri huyo alitoa agizo hilo katika eneo la ofisi hiyo iliyopo Mkokotoni, baada ya kufika na kuwaona abiria wengi wakiwamo wanawake, wanaume na watoto waliofungiwa ndani wakisubiri usafiri wa kuelekea Tanga. Hali hiyo ilimfanya waziri huyo kuchukua uamuzi huo kutokana na kubaini kuwa ofisi hiyo inasafirisha abiria kinyume na utaratibu na sheria zilizowekwa na serikali. Alisema hali hiyo haikubaliki na inaweza kusababisha hatari kwa maisha ya watu na serikali kupata lawama.

"Kwa mujibu wa kanuni ya 2007 ya usajili na leseni ya vyombo vidogo vya majini kifungu cha 105, inaelekeza vyombo vyote vilivyosajiliwa kwa abiria vichukue abiria na vya mizigo vichukue mizigo na sio kutumika kwa matumizi mengine mpaka amri itolewe na serikali," alisema.

Hata hivyo, Naibu huyo alisema, hakuna sababu kwa ofisi hiyo kuendelea kufanyakazi ya kuchukua abiria kinyume na taratibu na sheria zilizowekwa na serikali. Ahammada alieleza kwamba, serikali imerahisisha suala la usafiri katika maeneo tofauti ikiwamo safari za Zanzibar hadi Dar es Salaam, Pemba Zanzibar na Pemba Tanga, hivyo amewataka wananchi kuacha tabia ya kusafiri kwa vyombo visivyo rasmi.



Askofu wa Kanisa Katoliki jimbo la Zanzibar, Augustino Shaon, akiandika ujumbe kwenye mshumaa maalumu wa Pasaka, muda mfupi kabla ya kuanza Misa ya mkesha wa Pasaka jana, iliyoadhimishwa kwenye kanisa la St.Joseph mjini Zanzibar jana.
**PICHA: MARTIN KABEMBA.**

# Watoto waendelea kuzurura mitaani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Serikali ya Zanzibar kufunga shule na madrasa ili kuwaepusha watoto na mikusanyiko na kuwakinga dhidi ya maradhi ya corona, wengi wao kwa makundi wanaonekana mitaani wakicheza na kufanya biashara.

Nipashe ilishuhudia kundi kubwa la watoto wakiwa katika biashara ya kusafisha samaki kwa ajili ya kujipatia fedha katika eneo la soko la mnada wa Samaku,Unguja Ukuu Mkoa wa Kusini Unguja.

Muhammed Khatib Maulid, mkazi wa kijiji hicho, alisema kuwa tatizo la watoto kujishughulisha na biashara katika soko hilo ni jambo la kawaida na jamii ya kijiji hicho wamelikubali hawaoni athari za watoto kujihusisha katika biashara hizo za uvuvi.

Alisema hivi sasa baada ya serikali kutangaza shule na madrasa kufungwa, idadi ya watoto imeongezeka sokoni hapo.

"Kabla ya shule na madrasa hazijafungwa, watoto waliokua wakifika hapa ni kati ya miaka 14, lakini hivi sasa watoto wa miaka saba wapo sokoni hapa," alisema.

Alisema kuwa Sheha wa kijiji hicho anajitahidi kuwafukuza watoto hao, lakini jitihada zake bado hazijazaa matunda kwa sababu jamii haimpi ushirikiano mkubwa kuliondoa tatizo hilo.

Alisema watoto hao baadhi yao huwa na wazazi wao sokoni, bila ya kujali athari anazoweza kuzipata mtoto ikiwamo kukosa masomo. Aliwataka wazazi na walezi kuungana na Sheha wa kijiji hicho kuhakikisha watoto wanabaki majumbani mwao ili kujikinga na maradhi ya corona na watoto kuendelea kupata elimu kuliko kujiingiza mapema katika biashara ya uvuvi.

Naye Khadija Khamis, mkazi wa Kijiji cha Kitogani, alisema baadhi ya jamii haiamini kuwa ugonjwa wa corona upo kwa sababu watoto wapo katika mikusanyiko mbalimbali ikiwamo maeneo ya wazi wakicheza gololi, mpira na kujihusisha katika biashara ya uvuvi.

Aliviomba vyombo vya ulinzi na usalama kufanya doria mitaani ili kuwatawanya watoto ambao wapo katika mikusanyiko ili waepuke maambukizi.

Alisema corona haina maskini, tajiri, dini, siasa wala rika au jinsia hivyo ni vyema jamii ikachukua tahadhari na kuwalinda watoto wasiwe katika mikusanyiko.

Naye Sheha wa Shehia ya Unguja Ukuu Kaepwani, Khamis Vuai Shomari, alisema wimbi la watoto ni kubwa katika soko la mnada wa samaki kijijini hapo na aliwataka wazazi kuwakataza watoto wao wasiende katika eneo hilo kwa sababu wakiendelea kuwapo watapoteza malengo. Alisema watoto hupenda kwenda sokoni hapo kwa sababu wanapata pesa baada ya kusafisha samaki sasa wanaweza wakakatisha masomo kwa tamaa ya biashara hiyo.

# Wanawake watakiwa kuacha hofu nafasi za uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VYAMA vya siasa nchini, vimeshauriwa kuweka na kutekeleza sera maalumu itakayotoa fursa kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema bado kuna changamoto kubwa katika vyama vya siasa ambavyo havitoi fursa sawa kwa wanachama wake wanapotaka kugombea nafasi za uongozi.

Alisema vyama vya siasa licha ya kunadi uwapo wa sera ambazo zinawezesha wanawake kugombea nafasi za uongozi, hadi sasa zimekuwa zikiishia kwenye makaratasi na kushindwa kuzifanyia kazi.

Katika hatua nyingine, Naibu Spika huyo alisema, uwapo wa nafasi za viti maalumu kwa wanawake ni mfano wa kuwajengea uwezo wa kuingia kwenye mchakato wa majimbo na sio kubweteka wakiamini kuwa hawawezi.

Vile vile, alisema licha ya uwapo wa mwamko kwa baadhi ya wanawake kutaka kugombea nafasi za uongozi, hadi leo wengi wao hawafahamu nini wanachokitaka.

"Ili tuweze kufanikiwa ni lazima sisi wanawake tuweke malengo yetu kabla ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi ili tuweze kumshinda adui yetu," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Asha Abdalla Mussa, alisema wanawake wanaotaka kugombea nafasi za uongozi wana wajibu wa kufanya utafiti pamoja na kutengeneza ushawishi kivitendo kwa wajumbe wenye kutoa uamuzi ndani ya chama.

Mwakilishi huyo alitoa ushauri kwa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar muda ukifika wa kufanya kampeni kuwaandaa wale wenye mwelekeo wa kukubalika kwenye jamii.

Hata hivyo, amekiri kuwa kuna tatizo kubwa hususani Zanzibar kwa wanawake wengi kushindwa kujitokeza katika uchaguzi kutokana na hofu ya kupambana na wanaume kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti Baraza la Wanawake Chadema Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mwanamrisho Abama, alisema ipo haja kufanyiwa mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa na kuweka wazi uwapo wa nafasi za wanawake katika majimbo na si kwa nafasi za viti maalumu pakee.

# Serikali yahakikishia wananchi uwapo wa chakula cha kutosha

**Na Mathias Canal**

SERIKALI ya imeendelea kuhakikishia wananchi kuwa, nchi itaendelea kuwa na chakula cha kutosha ili watu wake wawe na nguvu ya kufanya kazi kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Kauli hiyo ilitolerwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, mwishoni mwa wiki mkoani Songwe wakati akikagua mashamba ya wakulima.

Akiwa katika Kijiji cha Idiwili na Iyula mkoani humo, Waziri Hasunga aliridhishwa na hali ya ustawi wa mazao ya wakulima, hivyo kuwahakikishia wananchi kuwa kutakuwa na mavuno ya kutosha katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020, kwani wakulima wengi wameitikia wito wa serikali wa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Waziri Hasunga alisema kwa miaka mitatu sasa serikali imeendelea kuhakikisha nchi inazalisha mazao mengi na ya kutosha ya chakula kutokana na kazi nzuri inayofanywa na wizara ya kilimo na taasisi zake.

Alibainisha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula mwaka 2019 ulishuka ikilinganishwa na mwaka 2018, ambapo nchi ilizalisha tani milioni 16.8, hivyo katika msimu huu wa mwaka 2020 nchi itazalisha mazao ya kutosha na kuwa na utoshelevu mkubwa wa chakula.

Aliwapongeza wakulima nchini kwa kuitikia wito na maelekezo ya serikali katika kuhakikisha uzalishaji nchini unaendelea kuongezeka hususani kwenye mazao ya chakula na biashara.

Katika hatua nyingine, Waziri Hasunga ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), kuhakikisha inaharakisha upatikanaji na usambazaji wa mbolea aina ya UREA ambayo imeadimika kwa wakulima.

Kadhalika, Waziri Hasunga amebainisha mkakati wa serikali wa kuongeza uzalishaji wa zao la pareto ambapo umeanza mkakati wa makusudi wa kuanzisha shamba la pareto katika Kijiji cha Idiwili mkoani Songwe kwa ajili ya uvunaji wa mbegu ili kuongeza kiasi cha mbegu kwani idadi ya wakulima inaongezeka kila siku.



Pamoja na Serikali kufunga shule kwa ajili ya hofu ya virusi vya corona, baadhi ya wazazi mjini Iringa wamewaachia huru watoto wao kwenda viwanja wa bustani ya Manispaa kucheza, kama walivyokutwa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Morogoro kinara idadi wenye ualbino

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKOA wa Morogoro unasadikiwa kuwa na idadi kubwa ya watu wenye ualbino ukilinganisha na mikoa mingine nchini.

Hali hiyo inatokana na Wilaya ya Kilombero pekee kuwa na watu 180 ambapo asilimia 70 kati yao wakidaiwa kuathirika na mionzi ya jua, hivyo kuwa hatarini kukumbwa na saratani ya ngozi.

Katibu wa Chama cha Wenye Ualbino Tanzania (TAS) mkoa wa Morogoro, Yasini kasiga, alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanyika wilaya ya Kilombero, imebainika asilimia kubwa ya wenye ualbino waliopo wapo hatarini kuathirika na saratani.

Kasiga alisema kwa mujibu wa takwimu zilizopo, mkoa wa Morogoro una watu 880 pekee waliotambuliwa kuwa na ualbino, takwimu zinazoelezwa kutoendana na uhalisia.

"Morogoro ni mkoa pekee unaoonyesha kuwa na idadi kubwa ya wenye ualbino ukilinganisha na mikoa mingine, pia kuna idadi kubwa ya mashambulizi ya jua kwa wenye ualbino kwa maana ya viashiria vya kansa ukilinganisha na mikoa mingine, hivyo ndio maana wenye ualbino Morogoro tupo hatarini," alisema Kasiga.

Aidha, Kasiga alisema hali ya kiuchumi inachangia kuwapo kwa changamoto kubwa inayokwamisha kufanyika utambuzi wa watu wenye ualbino na kufanya idadi yao kuoneka sahihi na kutoa elimu kwa jamii hiyo .

Alisema TAS kupitia ufadhili wa mradi wa kutoa msaada wa VOICE Global Tanzania wanakuja na mradi wa kuibua fursa kwa watu wenye ualbino mkoani hapa.

Mwenyekiti wa TAS mkoa wa Morogoro, Hassan Mikazi, alisema ni wakati sasa watu wenye ulemavu kuitumia fursa iliyopo kwa mwaka huu ya kujiingiza kwenye uchaguzi kutokana na kuwa ni mwaka wa uchaguzi na kuacha kulalamika baadae.

Alisema wenye ulemavu hawakuchagua kuzaliwa kama walivyozaliwa, hivyo hawanabudi kusaidiwa kufikia malengo kutokana na fursa zilizopo.

Mdau wa masuala ya ulemavu, Dk. Dustan Kamanzi, alisema wenye ualbino wana nafasi ya kujua mambo mbalimbali ikiwamo mikakati katika nchi kama bajeti, mazingira ya shule, usalama barabarani na mengine ili kuwalinda wenye ulemavu kwa ujumla.

Naye mwanahabari, Warioba Igombe, alisema kutokana na idadi kubwa ya wenye ualbino kubainika Ifakara, wadau hawanabudi kuwasaidia wenye ualbino kupambana na changamoto mbalimbali wanazokutana nazo.

# Wasiochukua tahadhari ya corona kutozwa faini

**Na Manuel Kaminyoge,** SONGWE

MKUU wa Wilaya ya Songwe mkoani Songwe, Samuel Opulukwa, ameagiza watu wasiochukua tahadhari ya corona kutozwa faini pamoja na hatua zingine za kisheria kwa kuwa wanahatarisha maisha ya wengine.

Alisema hayo baada ya Kamati ya Ulinzi na usalama ya Mkoa ikiongozwa na Mkuuu wa Mkoa, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela, kufanya ukaguzi wa utayari wa kukabiliana na corona.

Alisema kuwa wanawafuatilia wageni wote wanao toka nje ya wilaya waliopo katika nyumba za kulala wageni na kuchukua maelezo yao na kutoa elimu kwa umma.

Aidha, alisema kamati hiyo ilibaini baadhi ya mapungufu ambayo kama wilaya itasimamia kuyarekebisha itakuwa na madhara makubwa baadaye.

Kwa mujibu wa Opulukwa, eneo la kuwatenga washukiwa wa corona lina vitanda vya kutosha na kujenga kichomea taka katika Zahanati ya Saza ambayo itatumika kutibu wagonjwa hao.

"Sasa tunaanza kutoza faini wote wasiofuata maelekezo ya wataalamu wa afya kuhusiana na corona, mfano tukipita dukani au sehemu ya biashara na hakuna maji na sabuni, tutatoza faini na kufunga kwa muda biashara hiyo mpaka mtu huyo azingatie maelekezo hayo," alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Dk. Humphrey Masoke, alisema wameshaagiza vifaa kinga na tiba vyote muhimu katika Bohari Kuu ya Dawa ili kuongezea katika vifaa vichache walivyo navyo.

Dk. Masoke aliongeza kuwa wanaendelea kutoa maelekezo na elimu kwa jamii juu ya tahadhari kwa kuwa bado baadhi ya wananchi wanaamini ugonjwa wa corona ni wa Wazungu, hivyo hauwahusu.

Akizungumza na wananchi, Brigedia Jenerali mwangela alisema kuwa kila mwananchi achukue tahadhari ya kujilinda na kuwalinda wanaomzunguka.

# Papa aendesha misa ya pasaka kwa mtandao

**ROME,** Italia

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, amelazimika kuvunja mila ya karne kadhaa ya ibada ya Jumapili ya Pasaka kwa kuiendesha misa hiyo kwa njia ya mtandao badala ya kukaa na waumini kutokana na hofu ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Akiendesha ibada hiyo jana, ambaye mtu pekee aliyekuwa mbele yake alikuwa mpigapicha wake, Papa Francis alitoa wito kwa walimwengu kutokukubali kutawaliwa na hofu katika wakati huu dunia inapopambana na ugonjwa wa virusi vya corona na badala yake watambuwe kuwa giza na mauti sivyo vyenye kauli ya mwisho.

Papa Francis aliendesha misa hiyo akiwa kwenye maktaba yake binafsi ndani ya Kanisa la Mtakatifu Petro.

"Kwa wiki kadha sasa, tumeendelea kurejelea kauli kwamba, mambo yatakaa sawa, tukijiambatanisha kwenye uzuri wa ubinadamu na kuruhusu maneno ya kutia moyo kusimama kwenye nyoyo zetu," alisema Papa Francis na kuongeza:

" Lakini kadri siku zinavyokatika na hofu kuongezeka, ndivyo ambavyo hata wale majasiri kabisa wanavyoweza kujikuta wakivunjika moyo.

**Kwa wiki kadha sasa, tumeendelea kurejelea kauli kwamba, mambo yatakaa sawa, tukijiambatanisha kwenye uzuri wa ubinadamu na kuruhusu maneno ya kutia moyo kusimama kwenye nyoyo zetu.**

Tusitamauke.... Tunaweza na lazima tuwe na matumaini".

Kauli ya Papa Francis ilipongezwa na Waziri Mkuu wa Italia, Giuseppe Conte, kwa kile alichosema ni ishara yake ya uwajibikaji kwa kuadhimisha Pasaka akiwa faragha.

"Licha ya kuwa maneno yake yametamkwa mbali kutoka Uwanja wa Mtakatifu Petro, ambao kwa sasa umefunikwa na kimya cha kutisha, yamemfikia kila mtu," alisema waziri mkuu huyo wa taifa ambalo lenyewe limeshuhudia vifo vya makumi kwa maelfu ya watu.

Ibada hiyo inayowajumuisha pamoja waumini bilioni 1.3 wa Kanisa hilo ulimwenguni, inawakilisha kufufuka kwa Yesu Kristo, ambapo waumini mjini Roma walijaza keki mashuhuri za Pasaka siku kadhaa kabla, kuadhimisha sikukuu yao muhimu.

Siku ya Ijumaa Kuu, Papa Francis alifika kwenye uwanja mtupu wa Vatican akiwa amevalia joho lake jeupe ili kuuwasha mwenge wa kuashiria mwanzo wa ibada, lakini baadaye kiongozi huyo mwenye asili ya Argentina na mwenye umri wa miaka 83 alikiri kwamba hata yeye mwenyewe anajihisi kwamba ni kama vile yumo kwende tundu.

Kwa zaidi ya miaka 50, tukio hili lilikuwa likifanyika mbele ya hadhara ya watu wasiopunguwa 20,000, lakini tangu mwanzoni mwa Machi, mji wa Roma kama yalivyo mingine ya Italia, umekuwa kwenye zuio na kujitenga kutokana na athari za ugonjwa wa virusi vya corona.

Misa ya Jumapili ya Pasaka na kile kinachoitwa ujumbe wa baraka wa "Urbi et Orbi" vilihuhudhuriwa na watu 70,000 mwaka jana kwenye Uwanja wa Mtakatifu Petro.

Lakini kwa sasa lango la kuingilia makao makuu ya Kanisa Katoliki, Vatican, limefungwa na linalindwa na polisi wenye silaha waliovalia vifaa vya kujikinga na maambukizi usoni na mikononi mwao.

Kwenye mahojiano yake yaliyochapishwa na magazeti kadhaa ya Kikatoliki, Papa Francis alikiri wazi kwamba hata yeye anapambana kama mtu mwengine yeyote ili kukifanya kipindi hiki kiwe na maana maishani mwake.

Papa Francis alisema: "Tunapaswa kuishughulikia hali hii kwa kujitenga tukiwa na ubunifu. Ama tunaweza kupata mfadhaiko na kutengwa au tunaweza kuwa wabunifu zaidi." **DW**



Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, akiwa katika ibada ya pasaka. **PICHA: REUTERS**

## Mjadala Chloroquine tiba ya corona wapamba moto

**BEIJING,** China

MJADALA unaendelea nchi mbali mbali duniani juu ya dawa zinazotumiwa kwa muda mrefu kutibu malaria, Chloroquine zinaweza kuleta nafuu kwa wagonjwa wa virusi vya corona.

Mjadala huo umepata nguvu baada ya baadhi ya madaktari wa China na Korea Kusini ambako ugonjwa ulianzia kusema wagonjwa waliopewa dawa hiyo kwa mchanganyiko na dawa za 'antibiotics' wameweza kupona haraka.

Hata hivyo, waatalamu wengi wanatahadharisha wakisema uchunguzi zaidi wa kisayansi unahitajika kuhakikisha dawa hiyo inaleta mabadiliko. Daktari wa magonjwa ya kuambukiza, Didier Raoult, kutoka taasisi ya IHU mjini Marseille Ufaransa, alijiondoa kwenye tume ya taifa ya kupambana na corona baada ya kusema mwishoni mwa mwezi wa Machi majaribio ya chloroquine kwa wagonjwa 36 imepunguza idadi ya virusi mwilini.

Baada ya malumbano hayo, Raoult alitoa majaribio ya watu 100 na matokeo sawa. Akisisitiza kwamba walitumia pia dawa ya arithromycin dawa ya kawaida kupambana na mambukizi ya bakteria.

Waatalaamu wanabisha uchunguzi wa watu 34 hautoshi kusema ni utafiti wa kisayansi uliokamilika. Lakini Raoult anaamini ubishi unatokana na dhana ya kampuni ya dawa kuwa na tamaa ya kupata fedha nyingi. Didier Raoult, Mkurugenzi ya taasisi ya magonjwa ya kuambukiza ya Mediterranian, Ufaransa anasema : "Kuna hii hali ya shauku, ya lazima tupate dawa mpya. Lazima tupate chanjo mpya. Ukiwambia sikilizeni kuna hii dawa tunayoifahamu na inafanya kazi vizuri ya Cloroquine, na isiyo ghali, wanakataa. Ninadhani ni suala la fedha tu."

Kutokana na shinikizo la waatalamu, hivi sasa Ufaransa imeruhusu madaktari kutumia dawa hiyo kwa tahadhari katika hospitali peke yake.

Korea Kusini inatumia dawa hiyo kwa wagonjwa ambao wako taabani kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona na huko Prof.Kim Woo Joo wa magonjwa ya kuambukiza anatahadharisha pia utumiaji wake. **VOA**

# Waliofariki kwa corona Kenya yafikia wanane

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya watu waliofariki kutokana na janga la virusi vya corona nchini Kenya imefikia wanane, baada ya mtu mmoja zaidi kufariki nchini humo ndani ya saa 24 zilizopita.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Waziri wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, alisema kifo hicho kimetokea katika Jimbo la Siaya, Magharibi mwa Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kazi ya kutambua watu ambao walikutana na marehemu kabla ya kufikwa na umauti inaendelea.

Wakati huo huo, Waziri Kagwe ameeleza kuwa wagonjwa wapya sita wamethibitishwa nchini humo baada ya watu 766 kufanyiwa vipimo ndani ya saa 24 zilizopita.

"Kati ya wagonjwa hao, wanaume ni watano na mwanamke ni mmoja. Raia wa Kenya ni watano na mmoja ni raia wa kigeni," imeeleza taarifa hiyo na kuongeza:

"Wawili kati yao hivi karibuni walisafiri kutoka Mashariki ya Kati, mmoja ametokea Mombasa na watatu hawana historia ya kusafiri katika siku za hivi karibuni. Umri wao ni baina ya miaka 25 mpaka 59."

Alisema watano kati ya wagonjwa hao walikuwa kwenye vituo vya karantini ya lazima vilivyowekwa na serikali na mmoja alipatikana kwenye msako wa timu ya uangalizi. Wagonjwa hao wamepatikana katika majimbo ya Nairobi, Mombasa na Siaya.

Alisema habari njema ni kuwa, mtu mmoja amepona virusi hivyo na kufanya idadi ya waliopona Kenya kufikia 25.

Juzi, kulikuwa na wagonjwa wawili tu ambao walipatikana Kenya , huku wagonjwa 11 wakitarajiwa kuruhusiwa kwenda nyumbani baada ya kupona virusi hivyo nchini Rwanda.

Kiwango kilichotangazwa Jumamosi ni cha chini cha maambukizi kutangazwa na Wizara ya afya nchini Kenya tangu kutangazwa kwa mara ya kwanza kwa maambukizi ya virusi hivyo machi 13 ambapo mtu mmoja alitangazwa.

Katika tangazo lililotolewa na Katibu Mkuu wa wizara ya Afya, Mercy Mwangangi Jumamosi, wagonjwa wapya ni Mkenya mmoja na mwingine ni raia wa kigeni.

Ijumaa Kenya ilitangaza kuwa watu 10 waliokuwa wakipata matibabu ya virusi hivyo katika vituo vya kujitenga na hospitali ya Mbagathi wamepona na wataruhusiwa kwenda nyumbani. **BBC**



# POGBA: NINA NJAA YA KURUDI DIMBANI

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Paul Pogba, amesema "ana njaa sana" ya kurudi dimbani baada ya kuukosa kwa muda mrefu msimu huu kutokana na majeruhi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27, hajacheza tangu Desemba 26, mwaka jana, baada ya kujitonesha majeraha yake aliyoyapata mwanzoni mwa msimu huu.

Pogba ameliambia gazeti la Manchester kuwa "amepagawa kwa muda mrefu" kukosa kucheza lakini ataanza mazoezi wakati klabu itakaporejea dimbani baada ya mlipuko wa virusi vya corona kumalizika.

"Ni kama nipo pale; Nafikiri kuhusu mazoezi na timu," alisema.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia alifanyiwa upasuaji Januari na amecheza mechi nane tu msimu huu.

"Unafikiria vibaya, lakini kamwe sijawahi kuwaza hivyo, hivyo mara zote nakuwa kwenye hali ya kawaida," aliongeza.

"Inanifanya niwe na njaa ya kurudi na kufanya vizuri, na hiyo inanionyesha namna gani napenda soka."

Awali Ligi Kuu ya England iliahirishwa hadi Aprili 3 na baadaye Aprili 30 , mwaka huu, lakini sasa imebainishwa itarudi wakati hali itakapokuwa ya kuridhisha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# Mbappe atatua Madrid – Rothen

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe kujiunga na Real Madrid ni "suala la muda tu" kwa mujibu wa Jerome Rothen, ambaye amedai nyota huyo wa Paris Saint-Germain atatua kwa miamba hao wa LaLiga baada ya mlipuko wa virusi vya corona (covid-19).

Mbappe ameendelea kuhusishwa na Madrid, ambapo kocha Zinedine Zidane hajaficha siri ya kuvutiwa na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, aliondoka Monaco na awali alijiunga na PSG kwa mkopo mwaka 2017, na mkataba wake unamalizika mwaka 2022, lakini Mbappe hajaonyesha nia ya kuingia mkataba mpya na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Na sasa kiungo wa zamani wa PSG, Rothen, amesema Mbappe alikaribia kusaini Madrid kabla ya ugonjwa wa COVID-19, ambao umegharimu maisha ya watu zaidi ya 109,654 duniani kote.

"Najua kutoka nyanzo vyangu ndani ya klabu kwamba, mpango wa Kylian Mbappe kwenda Real Madrid ulikaribia kukamilika," alisema Rothen, ambaye alishinda mataji mawili katika kipindi cha miaka sita aliyokaa pale PSG, akiiambia Redio Montecarlo.

"Lakini kutokana na kile kilichotokea, nina uhakika safari ya Mbappe kwenda Real Madrid itaahirishwa."

Rothen aliongeza: "Hakuna njia kwamba Mbappe ataongeza mkataba pale PSG."



# Pele amtaja Ronaldo bora kuliko Messi



**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa Brazil, Pele, amejitosa kwenye mjadala wa kuwachambua nani bora kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, lakini anaamini yeye ni bora zaidi kushinda wawili hao.

Pele mwenye umri wa miaka 79, ambaye ameshinda Kombe la Dunia mara tatu na kufunga mabao 1281 katika kipindi chake cha uchezaji, anachukuliwa kama mchezaji bora wa soka wa wakati wote.

Kati yao Messi na Ronaldo kwa pamoja wameshinda mara 11 kati ya 12 kwenye tuzo za Ballon d'Or – sita akibeba Messi na tano Ronaldo.

Licha ya nyota wa Barcelona kumzidi tuzo mshambuliaji wa Ureno, Pele, anafikiri Ronaldo kwa sasa ndiye bora.

"Kwa sasa nafikiri Cristiano Ronaldo ndiye mchezaji mwenye kiwango kisichoshuka, lakini huwezi kumsahau Messi," alisema akiiambia televisheni ya mtandaoni ya Pilhado.

Mafanikio ya Pele yamekuwa yakishindanishwa na gwiji wa Argentina, Diego Maradona.

Alipoulizwa kama alikuwa bora zaidi kuliko Ronaldo na Messi, Pele alisema: "Hilo ni swali gumu kulijibu. Nimekuwa nikiulizwa mara nyingi.

HABARI MICHEZO

# Suarez kiduchu aondoke Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez alikuwa tayari kuondoka Barcelona kurudi katika klabu yake ya kwanza ya Nacional, wakati Sebastian Abreu, alipokaribia kupewa nafasi ya ukocha, amedai mchezaji huyo wa zamani wa Uruguay.

Nacional haikuwa na kocha mwaka jana wakati Alvaro Gutierrez alipojiuzulu, huku Abreu ambaye alicheza pale kwa misimu mitatu alikuwa na nafasi ya kuchukua nafasi hiyo.

Wakati huo Suarez alikuwa tayari kurudi kuichezea timu hiyo licha ya kwamba ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi kwenye Ligi Kuu ya Hispania akiwa na mkataba na Barcelona hadi mwaka 2021.

Abreu alikuwa mchezaji mwenzake na Suarez kwenye timu ya Taifa ya Uruguay kati ya mwaka 2007 na 2012, ambapo waliisaidia timu yao kumaliza nafasi ya nne kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2010.

"Nilikuwa na nafasi kubwa ya kuwa kocha wa Nacional," alisema akiiambia redio ya Uruguay, Sport 890."







# DE ROSSI ATAKA KUINOA ROMA

**ROME,** Italia

DANIELE de Rossi amebainisha kwamba malengo yake ni kuwa kocha wa AS Roma, hata kama itamchukua miaka 20 ijayo kupewa kazi hiyo.

Nahodha huyo wa zamani wa Roma alicheza mechi 616 kwa klabu hiyo kabla ya kwenda kucheza kwa muda mfupi Boca Juniors alikomalizia kipindi chake cha uchezaji.

Sasa akiwa na umri wa miaka 36, na akiwa amestaafu soka, De Rossi, hayupo tayari kuuacha mpira wa miguu nyuma na anaamini anaweza kuendelea kwa kuwa kocha.

Akizungumza na Sky Sport Italia, De Rossi alisema anatumaini kuwatembelea makocha kama wa Manchester City, Pep Guardiola kujifunza mengi kutoka kwake.

"Nataka kuwa kocha. Nimecheza kwa miaka 20 kwa timu moja na huwa haitokei kila siku. Hilo linaweza kutokea kama ukiwa kocha, hasa hapa Roma," alisema De Rossi.

"Siku moja ningependa kuinoa timu kama Roma, lakini kwanza natakiwa kuwa kocha."

# *Martinez anafaa zaidi Barc - Pizzi*

**MILAN,** Italia

NYOTA wa Inter Milan, Lautaro Martinez, atakuwa "mshambuliaji sahihi" kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Barcelona, kwa mujibu wa Juan Antonio Pizzi.

Martinez ameripotiwa kutakiwa na Barca, huku miamba hao wa Hispania wakiwa na nia ya kumfanya kuwa mrithi wa muda mrefu wa mshambuliaji mkongwe, Luis Suarez.

Wapinzani wa Barca kwenye LaLiga, Real Madrid pia wanahusishwa na mpango wa kumuwania nyota huyo, huku Manchester United na Manchester City kutoka Ligi Kuu ya England zikitajwa pia kumtaka.

Mshambuliaji wa zamani wa Barca, Pizzi, ambaye amewahi kuzinoa Chile na Saudi Arabia, ametaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 22, kutua pale Camp Nou.

"Lautaro Martinez ni zaidi ya Kun (Sergio) Aguero ni aina ya mshambuliai atakayefiti zaidi kucheza Barca," alisema Pizzi mzaliwa wa Argentina ambaye ni raia wa Hispania akiiambia EFE.

"Tayari ameshajithibitishia yeye mwenyewe nini anachoweza kufanya na Argentina, Racing na Inter. Anaonyesha kuwa mshambuliaji atayefiti zaidi pale Barcelona hasa kwa staili yao ya uchezaji.

Martinez aliondoka Racing Club na kujiunga na Inter mwaka 2018 na tayari amejithibitishia ubora wake kama mmoja wa washambuliaji bora duniani.

Amefunga mabao 25 tangu amejiunga na Inter akitokea Racing Club ya Argentina.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# 'AUBAMEYANG SASA JIONDOKEE ARSENAL'

●●● Kwa sasa yupo Arsenal, na hajashinda chochote pale, akipata klabu yenye malengo, atakuwa...

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal Pierre-Emerick Aubameyang, anahitaji "kupata mkataba na klabu yenye malengo zaidi," amesema Rais wa Shirikisho la Soka la Gabon, Pierre Alain Mounguengui.

**Straika huyo alimaliza msimu uliopita akiwa mfungaji bora pamoja na wachezaji wengine wawili kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na mabao 22.**

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21 pale Arsenal.

"Kwa sasa yeye yupo Arsenal, na hajashinda chochote pale, hivyo ni kama ameshindwa kutimiza malengo yake," alisema Mounguengui akiiambia ESPN.

"Sisemi kwamba klabu ya Arsenal haina malengo, lakini Arsenal haina malengo makubwa kama klabu nyingine za Ulaya zilivyo."

Mwezi uliopita kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, alisema anataka kumbakisha Aubameyang "kwa hali yoyote" na anahitaji klabu kujadili mkataba wake mpya kabla ya mwishoni mwa msimu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon, amefunga mabao 20 kwenye mashindano yote msimu huu kwa 'Washikabunduki' hao na ameripotiwa kutakiwa na klabu kadhaa Ulaya zikiwamo Barcelona na Inter Milan.

"Kama Pierre akipata mkataba na klabu yenye malengo, atakuwa na nafasi nzuri zaidi," aliongeza kusema Mounguengui.

"Watu wote wa Gabon wanamuona Aubameyang yupo daraja la juu, ambapo sasa anaweza kumaliza kipindi chake cha uchezaji akiwa na klabu kubwa, tuzo binafsi na mataji."

Tangu ajiunge na Arsenal kwa ada ya pauni milioni 56 akitokea Borussia Dortmund Januari mwaka 2018, Aubameyang ameshuhudia wakifungwa kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa na lile la Carabao na bado hajashinda taji lolote.

## ZISIKUPITE

### LIVER WALIMTAKA ODEGAARD

KLABU ya Liverpool ilijaribu kumsajili kiungo wa Norway mwenye umri wa miaka 21, Martin Odegaard, kipindi cha majira ya joto kilichopita, kabla hajasajiliwa Real Sociedad kutoka Real Madrid, kwa mujibu wa kocha wake wa zamani Leonid Slutsky. ***(Metro)***

### NYOTA NIGERIA ATAKIWA EPL

KLABU za West Ham na Crystal Palace wanamwania mshambuliaji wa zamani wa Sunderland, Josh Maja mwenye umri wa miaka 21, kutoka klabu ya Bordeaux kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Sun on Sunday)***

### LIVER YAJITOA KWA SANCHO

KLABU ya Liverpool, imejitoa kwenye mbio za kumuwania nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho(20), na kuiacha Manchester United ikiwania kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye thamani ya pauni milioni 88. ***(Football Insider)***

### UPAMECANO AGOMBEWA EPL

KLABU za Ligi Kuu ya England zinamuwania mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 21, zikiwamo Arsenal, Tottenham na Manchester City, huku pia miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid wakimnyatia mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21. ***(Sunday Mirror)***

### UNITED KUMPOTEZA IGHALO

MCHEZAJI wa zamani wa kimataifa wa Nigeria, Abdul Sule, amesema Manchester United wanaweza kumpoteza Odion Ighalo mwenye umri wa miaka 30, kwa moja ya washindani wao Ulaya, kama hawatampa mkataba wa kudumu mshambuliaji huyo kutoka Shanghai Shenhua ya China kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Goal)***

### JUVE, UTD KWA RODRIGUEZ

WAKALA wa James Rodriguez, amezungumza na Manchester United na Juventus juu ya uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye umri wa miaka 28 kipindi cha majira ya joto kutoka Real Madrid.***(AS)***

### AONGEZWA MKATABA

KIWANGO cha Nemanja Matic alichokionyesha hivi karibuni, kimeifanya Manchester United kumpa mkataba mpya kiungo huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 31. ***(Daily Mail)***

### KUPEWA MKATABA MPYA

KLABU ya Coventry City inajipanga kumpa mkataba mpya kiungo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 23, Zain Westbrooke, ambaye amekuwa akihusishwa na klabu ya Derby County. ***(Derby Telegraph)***

### KONDOGBIA KUITOSA VALENCIA

MCHEZAJI Geoffrey Kondogbia wa Valencia, anayewaniwa na Tottenham, huenda akahamia katika timu nyingine kwa mshahara mdogo kuliko anaolipwa sasa, ikiwa klabu yake hiyo ya Hispania itashindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

### CHELSEA KUIPIKU ARSENAL

CHELSEA ina matumaini ya kufikia makubaliano na mlinzi wa Lille, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, kwa malipo ya takriban pauni milioni 30 ili kumsajili mchezaji huyo wa Brazil, ambaye pia ananyatiwa na Arsenal na Everton. ***(Express)***

# TSHABALALA AIONA SIMBA FAINALI CAF

**Na Saada Akida**

NAHODHA msaidizi na beki wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', amesema mipango yake ni kuona timu hiyo siku moja inacheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Tshabalala alisema anachotakiwa kukifanya ili Simba ifike hatua ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), ni kujituma na kuonyesha ushirikiano mkubwa kwa wachezaji wenzake.

**Alisema anaamini hilo litatimia kwa kuwa yupo pamoja na wachezaji wenzake katika kufikia malengo hayo.**

"Kila mchezaji hapa kwetu anahitaji kuona mafanikio, kubwa ni kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa, hali hiyo inatulazimu tupambane kuhakikisha tunachukuwa ubingwa na kujipanga kwa michuano hiyo ya kimataifa," alisema Tshabalala.

Alisema kwa sasa anapigania kuonyesha ushirikiano mzuri na wenzake katika kufikia malengo yao hayo akiamini kujituma kwao kutawezesha kuwapa mashabiki kile wanachokitarajia.

"Kwa kipindi hichi cha mlipuko wa virusi vya corona, tupo makini sana kwa sasa, nafanya mazoezi binafsi kwa kufuata maelekezo ya benchi la ufundi huku nikijilinda na kuzingatia yale yaliyokatazwa na wizara ya afya," alisema Tshabalala.

**PAMOJA SANA...**



Kipa wa Simba, Aishi Manula (kushoto), akimkaribisha mshambuliaji wa Azam FC, Shaaban Chilunda, kucheza naye 'game' nyumbani kwake, Chamazi, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, katika kipindi hiki timu zao zikiwa zimesitisha mazoezi kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). Manula na Chilunda wote wamewahi kucheza pamoja Azam FC baada ya kuibuliwa kwenye akademi ya klabu hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mwambusi aja na mbinu ligi kurejea



**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa zamani wa Mbeya City, Juma Mwambusi, ameibuka na kudai ni bora Ligi Kuu ianze ili kuondoa hofu iliyopo kwa sasa kutokana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), huku akitaja mbinu mbadala ya kuweza kurejea.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka mkoani Mbeya, Mwambusi (pichani) alisema Shirikisho la Soka nchini (TFF), linapaswa kuruhusu Ligi Kuu iendelee huku kila mchezaji akipimwa afya kuhakikisha hana maambukizi ya virusi vya corona.

"Ligi iendelee ili kuondoa wasiwasi uliopo sasa hivi kuliko kukaa kimya, mashabiki wanapaswa warudishe furaha, tunajua Watanzania wengi wanapenda mpira," alisema Mwambusi.

Aidha, kuhusu kucheza bila kuwapo kwa mashabiki uwanjani, Mwambusi alisema kutaathiri klabu, kwa kuwa nyingi zinategemea mapato ya getini kujiendesha.

"Mechi kuchezwa bila mashabiki hapa kwetu itaathiri klabu nyingi, mashabiki waruhusiwe kuingia uwanjani kwa kupewa utaratibu wa kukaa mbalimbali ili kujikinga na janga hili," alisema.

Mwambusi alisema wachezaji kukaa mwezi mmoja bila kusimamiwa na mwalimu katika mazoezi ni tatizo, na kwamba wengi wanakosa umakini na badala yake wanapoteza viwango vyao. Aliwataka wachezaji wote wawe makini kufuata maelekezo waliyoachiwa na walimu wao, ili kuiweka sawa miili yao.

## Hererima kutoangalia majina usajili KMC

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya KMC FC, Haruna Hererima, amesema hatasajili mchezaji yeyote kutokana na ukubwa wa jina lake, bali atamulika ambao wanaweza kuleta ushindani katika kikosi chake.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Hererima alisema ataanza usajili baada ya msimu huu kumalizika, endapo ligi hiyo iliyosimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), itaendelea.

"Nitasajili wachezaji ambao wataleta ushindani katika kikosi changu, sitaangalia ukubwa wa jina najali kiwango bora, alisema Haruna.

Alisema amewapa programu maalumu wachezaji wake wakiwa mbali katika kipindi hiki cha mapumziko ili kuiweka sawa miili yao.

Kwa upande wa Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Walter Harisson, amesema wanafuatilia mazoezi yanayofanywa na kila mchezaji, kwa umakini mkubwa.

"Lazima tuwafuatilie kwani bila kufanya hivyo watajisahau na kujikuta ligi ikianza wanaanza upya," alisema Walter.

Katibu huyo alisema mikakati yao ni kuifikisha mbali timu yao, ikiwa pamoja na kuhakikisha inarudisha makali yake.

"Tunataka kurudisha makali yetu pindi ligi itakapoanza, kila mchezaji ametuahidi kurudi na morali ya juu," alisema.

## Gwambina yaahidi mapinduzi Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema kikosi chake kinakuja kufanya mapinduzi makubwa ya soka msimu ujao wa Ligi Kuu Bara.



Akizungumza na Nipashe jana, Kocha huyo alisema anajivunia kuwa na kikosi imara kitakacholeta mapinduzi makubwa katika ligi hiyo.

Alisema kinachompa jeuri ni baada ya kupata uzoefu mkubwa kutoka kwa timu za Ligi Kuu ambazo wamecheza nazo katika mechi za kirafiki na mashindano ya Kombe la Shirikisho, FA Cup.

"Tunamategemeo makubwa ya kucheza Ligi Kuu, tunaenda kufanya mapinduzi kwani ukiangalia kikosi changu kipo vizuri kulingana na uzoefu wachezaji wangu walioupata."

"Ukiachilia mbali wachezaji niliokuwa nao, ninao ambao wamewahi kucheza Ligi Kuu na kuwa na uzoefu mkubwa na hata kuwahi kuzifunga hizi timu kubwa," alisema Fulgence.

# Michezo

Jumatatu Aprili 13, 2020

Nipashe





‘Aubameyang jiondokee Arsenal’ UKURASA 22

## Sababu Hazard kuchemsha Real

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amekuwa na wakati mgumu katika mwaka wake wa kwanza kucheza Madrid...



HABARI UK. 14

## Pele: Messi? Ronaldo bora

**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa Brazil, Pele, amejitosa kwenye mjadala wa kuwachambua nani bora kati ya Cristiano...



HABARI UK. 20

PALEE...



Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck (kushoto), akitoa maelekezo kwa msaidizi wake, Selemani Matola katika mazoezi ya timu hiyo kabla ya michezo kuzuiwa kwa mwezi mmoja kuanzia Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19). **PICHA: MAKTABA**

# Sven aanika Simba ijayo

## ●●● Asema mashabiki wanataka wapinzani wachezee hata tano, lakini yajayo yanafurahisha...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akieleza kufurahia ushirikiano na wasaidizi wake, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema anaamini utaleta mafanikio makubwa klabuni hapo na kuwataka mashabiki watarajie soka la kuvutia zaidi na kushambulia kwa kasi.

**Sven ambaye amerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems, katika kikosi hicho cha Simba anasaidiwa na makocha wazalendo Selemani Matola (msaidizi namba moja), Kocha wa Makipa, Muharami Mohamed na Kocha wa Viungo, Mtunisia, Adel Zrane.**

Benchi hilo la ufundi, linakamilishwa na Daktari Mkuu, mzawa Yassin Gembe na Mtaalamu wa Tiba ya Viungo, Mjerumani Paulo Gomez Dardenne.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Sven alisema, haikuwa kazi nyepesi kwake kuendana na wasaidizi wake hao, kwani mwanzoni ilimuwia vigumu kidogo, lakini kwa sasa kila kitu kipo vizuri na kwamba wanaisuka timu hiyo kwa ushirikiano mkubwa.

“Mwanzoni haikuwa rahisi, lakini kwa sasa hata ukiangalia utaona tunashirikiana sana na kila kitu kinafanyika vizuri,” alisema

Kuhusu mashabiki wa timu hiyo kutofurahishwa na ushindi mwepesi wanaoupata katika baadhi ya mechi, Sven alisema ni suala la muda tu kwa kuwa kwanza walianza kwa kuijenga timu kucheza soka la kuvutia.

Alisema awali alilazimika kutumia mshambuliaji mmoja wakati alipojiunga na Simba kwa sababu Meddie Kagere alikuwa straika pekee kikosini kutokana na wengine kuwa majeruhi.

“Kagere peke yake ndiye alikuwa mzima, lakini baada ya kupoteza mchezo dhidi ya JKT Tanzania, niliamua kucheza na washambuliaji wawili kwa sababu wachezaji wengine waliokuwa majeruhi walikuwa wamepona,” alisema kocha huyo aliyejiunga na Simba Desemba 12, mwaka jana baada ya kuachana na timu ya Taifa ya Zambia.

Alisema kwa sasa ameitengeneza timu hiyo kucheza soka la kushambulia kwa sababu asilimia 65 ya wachezaji wa Simba ni washambuliaji na anaelewa mashabiki wa timu hiyo kiu yao ni kuona wakishinda 3-0 bila na zaidi, lakini anachotaka ni kuijenga kucheza soka la kuvutia kwanza.

Hadi Ligi Kuu inasimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), Sven ameiwezesha Simba kukaa kileleni ikiwa na pointi 71 ikifuatiwa na Azam FC alama 54 baada ya kila moja kushuka dimbani mara 28, huku Yanga iliyocheza mechi 27 ikiwa katika nafasi ya tatu na alama zake 51.

Hata hivyo, safu ya ushambuliaji ya Simba inayoongozwa na Kagere aliyepo kileleni mwa orodha ya wafungaji akiwa na mabao 19, ndiyo inayoongoza kwa kucheka na nyavu mara nyingi ikiwa na mabao 63 hadi sasa.

Lakini pia licha ya safu ya ulinzi ya Simba mara nyingi hukosolewa kwa kufanya makosa, ndiyo inayoongoza kwa kuruhusu mabao machache (15) tu hadi sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >